

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**

**BARINGO CENTRAL CONSTITUENCY,**

**AT**

**KARBARNET COUNTY HALL**

**ON**

**4<sup>TH</sup> JULY 2002**

**RECORD OF THE PROCEEDINGS OF THE CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION PUBLIC HEARING IN BARINGO CENTRAL CONSTITUENCY AT KABARNET COUNTY HALL ON 4<sup>TH</sup> JULY 2002.**

**Present:**

Com. Pastor Zablon Ayonga  
Com. Zein Abubakar  
Com. Phoebe Asiyu  
Com. P.M. Wambua

**Secretariat staff in attendance:**

Fatuma Jama	Programme Officer
Makomere Wambeyi	Ass. Programme Officer
Lydia Moraa	Verbatim Recorder
Elijah Ndagula	District Cordinator

**Elijah Ndagula:** Commissioners wetu wa Constitution of Kenya Review Commission, viongozi wa Kabarnet, Baringo Central, wananchi watukufu, leo ndiyo ukingo wa kazi yote ambayo tumekuwa tukifanya kwa sababu ndiyo siku ambayo Commissioners watakuja kuchukua maoni yetu kama watu wa Baringo Central, ili kutumia kwa kuchangia uundaji wa katiba mpya ya nchi yetu.

Kwa hivyo kama inavyokuwa desturi yetu, tutaanza mkutano huu wetu kwa maombi. Kwa hivyo ningempa nafasi hii Pastor yeyote, mama kama anaweza kutuomba, atuombee ili tupate kuanza mkutano huu wetu wa kuchukua maoni.

**Mama Elizabeth Chesire: (Prayer):** Tuombe. Baba wetu wa mbinguni, muumba wetu, Baba wa Mwokozi wetu Yesu

Kristo, tumekuja miguuni pako mungu wetu asubuhi ya leo, kwa tarehe ya leo, mwezi huu wa saba hapa, ofisi yetu ya County Council Baringo Central.

Mungu asante sana Baba. Asante kwa ulinzi wako, asante kwa uongozi wako mwema, umetuongoza tangu tuzaliwe sisi wakubwa na wadogo.

Sasa Mungu wetu, sisi tuko hapa kama watoto wako na tena kama viongozi wa kuja kushughulikia mambo ya katiba yetu ya Kenya nzima. Sasa Mungu wetu tunakuja miguuni pako kuuliza usaidizi wowote kutoka kwako, mawazo yote mazuri kutoka kwako, halafu sisi tupate kutunza nchi yetu ya Kenya, kwa uwezo wako na uongozi wako mwema.

Sasa baba yetu asante kwa viongozi wetu wale umewatuma kutoka mbali, umewapa kazi hii kuongoza, uwalinde na kuwabariki. Na tena hata tunakumbuka Rais wetu mahali popote alipo, msaidie na kumbariki, kwa maana yeye ni kiongozi wa Kenya.

Mungu tubariki sisi zote, hata wale wangali bado wanakuja, waongoze na umpe kila mtu ujasiri ya kusema maneno ya kutosha sisi zote tuseme Amina. Mungu wetu ninaomba hayo machache katika jina la Yesu Mkombozi wetu.

**Elijah Ndagula:** Kama vile mnavyojua, Tume ya kurekebisha katiba ya Kenya wakati huu inazunguka katika nchi yetu kusanya maoni ili kuchangia kwa kuunda katiba mpya ya nchi yetu. Wakati huu wameshazunguka katika provinces zote na mkondo huu ni wa Rift Valley Province. Halafu baada ya kumaliza Rift Valley, ambako tunatarajia itakuwa wiki ijayo, wataenda upande wa Western Province ili wamalize kazi hiyo ya kusanya maoni kutoka kwenye constituencies.

Baada ya hayo wataenda kukaa chini na waandike katiba mpya, wakitumia maoni ambayo mtakuwa mmechangia kama wananchi katika kila constituency yetu nchini.

Kwa hivyo kama sijawapa Commissioners nafasi hii waendeleo na kazi yao, na wafanye introduction halafu waanze kazi, ningependa tu kuwajulisha kwamba tuko na committee ambayo inaitwa Constituency Constitution Committee, yaani 3C, ambao wamekuwa wakinisaidia kufanya kazi hii katika constituency yetu yetu.

Kwa upande wa Salawa tumekuwa na councillor Cherambus akiwa kwa hiyo committee, upande wa Kabarnet tumekuwa Mayor Kiprono, pia upande wa Tenges tumekuwa na Pastor Raimoi, halafu upande wa Marigat tumekuwa na Caronent Buru, pia tumekuwa na wakili wetu Bwana Kenei, tumekuwa na Mama Leah Tuikong', tumekuwa pia na Bwana Hosea Kiplagat na Bwana Richard Chebon upande ule mwingine.

Kwa hivyo wao ndio committee members na nataraji tukiendelea watakuja na baadaye tutakuwa na nafasi ya kufanya introduction. Kwa hivyo nafasi hii nitampa Commissioner Pastor Zablon ili atufanyie introduction ya Commissioners ambao wako hapa, na pia afanye introduction kwa DC wetu ambaye nimemwona kuwa ameingia na Mayor wa Kabarnet. Kwa hivyo nafasi hii nampa commissioner.

**Com. Pastor Ayonga:** Ningelipenda kuwauliza Bwana DC na Mayor waje hapa mbele na Clerk wa Council kama yuko hapa.

Nadhani kabla ya mimi ku-introduce Commissioners na staff ambao tumetoka nao ofisini, ningalipenda kumwuliza Bwana DC atukaribishe, tuko district yake na Bwana Mayor atukaribishe, kwa maana tuko katika County Hall yake, yeye na Clerk of the Council, ndipo tutajisikia kwamba tumekubalika hapa ndipo tuendelee.

**District Commissioner:** Asante sana Bwana Commissioner, Commissioners ambao wako hapa, Msahiki Mayor, viongozi na wananchi, ningependa kuchukua nafasi hii niwakaribisheni hapa Kabarnet. Ninafikiri mmezunguka na ni kama siku ya tatu katika sehemu hii. Karibuni, tumekuwa tukitarajia, wengi wamekuwa wakiongoja ili waweze kupatiana maoni yao. Kwa hivyo tunashukuru mmepata nafasi, wananchi mna uhuru ya kupatiana maoni. Karibuni. Asanteni sana.

(Applause)

**Com. Pastor Zablon Ayonga:** Bwana Mayor.

**Mayor:** Commissioners ambao mmekuja ili kusikiza maoni yetu kuhusu katiba ya nchi hii na DC na Clerk, viongozi, mabibi na mabwana, hamjambo?

(Applause)

Basi nami kwa niaba ya viongozi wa Baringo ya Kati, ninachukua nafasi hii kuwakaribisha katika town yetu na vile vile katika constituency yetu kwa ajili ya kazi iliyo mbele yetu. Kwa hivyo Commissioners, mjisikie mko nyumbani. Pia, ninataka kuungana na Bwana DC kwamba sisi tumekuja hapa, kwa ajili ya kutoa maoni yetu kuhusu katiba ya nchi yetu. Hii ni mara ya kwanza sisi, nafikiri kwa sisi zote tuliohapa ndani kupata nafasi kutoa maoni kuhusu jinsi katiba yetu tunavyotaka.

Kwa hivyo ni siku ya muhimu sana na ni jambo la muhimu sana kwamba wakati tunatoa maoni, tutoe maoni kwani katiba ambayo itakayoandikwa kutokana na maoni yetu ni katiba ambayo itaendesha nchi kwa miaka mingi ijayo kwa hivyo tunashukuru sana kwa sababu tumepata nafasi.

Labda siyo rahisi kupata nafasi ingine kama hii hata kwa miaka mingine, labda sisi tutatoka dunia hii bila kupata maoni mengine.

Kwa hivyo ni wakati wa maana sana nitoe maoni ambayo itaongoza nchi yii na kutuendesha kwa njia iliyo bora.

Kwa hayo machache ninachukua nafasi hii tena kusema asante, mjisikie nyumbani na mtoe maoni bila woga, bila kufikiri kwamba maoni ni ya watu fulani. Asante sana, na Mungu awabariki sana.

(Applause)

**Com. Pastor Ayonga:** Ninawashukuru Bwana DC na Bwana Mayor kwa kutukaribisha. Tumekuwa na wakati mzuri sana katika hii district yako Bwana DC, we have had maoni mazuri sana, tumekuwa na mikutano mizuri ambayo tukitoka hapa tutasema hatakuwa na incidence yoyote, hatakuwa na walevi wowote, lazima iwe Bwana DC, hii sehemu umeitunza vizuri sana,

watu hawanywi pombe.

(Applause)

Maanake tumepata watu ambao ni mature people, who have come to give there views and they have given us very mature views, ya kuweza kurekebisha katiba yetu.

Kwa niaba ya Commissioners ambao niko pamoja nao, tumechukua muda huu kama muda mzuri sana ambao tumekuwa nao katika Baringo na pia tunatumaini kwamba leo pia tutakuwa na mkutano mzuri hapa Baringo.

Tunayo sehemu moja ambao kesho tutakuwa, Mogotio, na kazi yetu ya Rift valley ya North, ya Kaskazini, itakuwa imeishia hapo.

Si sisi tu ambao tuko hapa Rift Valley ya Kaskazini, Commissioners wote, tuko vikundi nane na hivi vikundi nane vimetawanywa kote katika Rift Valley ya Kaskazini na kesho tutamaliza na wiki ijayo tutaenda Rift Valley ya Kusini na baadaye tutamaliza kazi ya Rift Valley tarehe kumi na saba mwezi huu ndipo tutaenda Western Province.

Lakini kwa vyovyote, tumekuwa na maoni mazuri na jinzi ambavyo Mayor alisema, hatuwezi kupata nafasi tena ya namna hii ya kutoa maoni. Huu ni wakati wa namna ya pekee na tena sisi wale ambao tuko hai na ambao tutatoa maoni, tutasema kwamba tulichangia kikamilifu katiba ya Kenya.

Kwa hivyo leo tunatazamia maoni yale yatachangia kurekebisha katiba. Ili nisipoteze wakati, ninataka kuwa-introduce Commissioners ambao niko pamoja nao na nitawapa nafasi wawasalimu pia.

Hapa mkono wangu wa kushoto ni Bi. Phoebe Asiyu. Phoebe Asiyu natumaini anajulikana na wengi kwa maana nimeona wamama wengine hapa wanamsalimu namna ya pekee, tena ninasikia yeye ni shemeji wa upande huu na yeye atakuja kuwaambia ushemeji wake, na ni politician wa zamani.

Politicians wale ambao wamekomaa, yeye si dot.com, yeye ni politician wa zamani. Yuko hapa na atakuja kuwasalimia na mtakuja kukubaliana nami kwamba ni politician aliyekomaa.

Mkono wangu wa kulia hapa karibu ni Commissioner Paul Wambua. Yeye si Commissioner tu lakini yeye ni mwana sheria na yeye nitampa nafasi awasalimu. Na kule mwisho na si mwisho tu, ni Commissioner Abubakar Zein. Huyu Abubakar Zein ni a Jack of all trades, mara ni Mwalimu, mara ni mwandishi, mara ingine sijui ni nini, lakini ni mtu mwema sana ambaye anachangia katiba hii kwa namna ifaavyo na yeye pia, huyu mwana Mombasa, mwana pwani, nitakuja kumpa nafasi naye awasalimu.

Na wakisha wasalimu, kabla hawajawasalimu, pia kutoka ofisi tunao staff ambao wanafanya kazi. Mmoja wao ni programme officer ambaye ni Bi. Fatma, yuko kule, Fatma simama ili wakuone. Huyu ndiye anayeongoza programme zetu hizi za kuzunguka na kuona kwamba kila jambo na zile memorandum zenu hakuna hata moja itapotea. Halafu nina vijana wawili, Makomere simama. Huyu kijana anaandika kama typewriter, mkono wake unaenda namna hivi, kila neno mnalosema linaangukia kalamu yake. Hiyo isitoshe, kwa maana hatuwezi kuamini mkono wa mtu, tuna Binti hapa ambaye anaitwa Mora, a

Moraa simama, huyu Binti ana kumashini kile ambacho kina-record. Hakuna neno la mtu ambalo litapotea wakati umekuja kuchangia. Hata ukikohoa tutachukua kikohozi chako na tutakuambia mzee au mama, si ni wewe huyu uliyekuwa unakohoa? Sasa leo unageuka namna gani?

Kwa hivyo katika hii kazi yetu hapa leo, kila neno litaandikwa. Mnapotuona hapa Commissioners, nasi tunaandika makubwa makubwa. Msije mkafikiri mbona yule sasa haandiki? Maneno yale yangu nilikuwa nayasema mimi kumbe hayakuwa na maana? Mambo yako kule, mambo yako hapa chini, yanaandikwa na yananaswa. Kwa hivyo tunatumaini kwamba mtachangia katika siku ya leo kwa katiba yetu.

Hebu nimpe Bi Asiyo nafasi awasalimie kwa kifupi ndipo Commissioner Wambua na Commissioner Zein pia wawasalimu.

**Com. Hon. Phoebe Asiyo:** Asante sana Pastor Ayonga, Commissioner

(Applause)

kwa kunipa nafasi hii ya kuwasalimia watu wa Kabarnet. Bwana DC, Bwana Mayor, Bwana Clerk, wale wakuu wa 3C's, wale ambao wamekuwa wakiendesha civic education na wale wote ambao wamehudhuria mkutano huu wa leo, tunawakaribisha kwa hamu sana na tunangojea kusikilisa maoni yenu juu ya katiba mpya, tukijua kwamba maoni yenu yatajenga Kenya mpya na kwamba maoni yenu yanaweza kuleta Kenya, watu wa Kenya waanze kufikiria zaidi kama ndugu.

Waliletwa na Mungu kuishi kwa nchi moja, hata kama hawasemi lugha moja, hata kama hawana culture moja. Lakini kiroho tutakuwa watu moja tukitengeneza katiba mzuri ambao itatuleta karibu; itatufanya tuwe marafiki na itakabhidhi mambo yote ambayo ile katiba ya zamani, ile ambayo hatukuchangia, tuliandikiwa na watu wa Britain.

Na wale watu wetu ambao walikwenda huko kuchukua hiyo katiba ambao bado wako wanaishi tuwape heshima na tuwape asante sana kwa kwenda huko Ulaya kuchukua hiyo katiba ambayo imetuongoza kwa miaka karibu arobaini. Na kwa kweli imetuongoza vizuri lakini hiyo nyumba, maana katiba ni kama nyumba ya mzee, wazee wa Kenya hawakujenga ilijengwa na wazee wa Ulaya. Sasa hivi leo tumepata nafasi, wazee wetu, kina mama wetu, vijana, tujenge nyumba mpya ya Kenya ambao watu wote wa Kenya wataweza kuishi kwa amani, kwa mapenzi na kwa umoja.

Na unajua, katika nchi nyingi sana hapa Africa, katiba hairekebishwi isipokuwa kukiwa na shida kama vita, kama kukosana na watu, kama kuna machafuko, ndiyo watu wanakaa chini wanatengeneza katiba mpya ya kuwalinda. Kwa hivyo mjione kama watu wana bahati sana, mnatengeneza katiba hali hakuna vita.

President yule ambaye walianza katiba hii bado yuko hai. Presidents wengi hawatengenezi katiba kama bado wanaishi, ni wachache sana. Kwa hivyo mjione mlio na bahati kubwa sana kwa nchi hii yetu ya Kenya na tumsifu Mungu kwa maana ametuwesha kufika na kutengeneza katiba ambayo itatusaidia kwa miaka mia moja ijayo.

Kwa hivyo kama utaongea, uongee ukijua si ya leo au kesho pekee yake, lakini hata miaka hamsini ijayo, katiba hii hii ambayo

mnatengeneza leo itashika nchi hii na itakuwa ndiyo sheria kuu ya sheria zote ambazo zitalinda maisha ya watu wa Kenya.

Ninawapa asante sana kwa kufika, tunatumainia kwamba mtatupatia mawaidha mema ambayo yatatusaidia sisi kuandika katiba kwa maana sisi hatuna maoni, maoni ni yenu, ninyi ndio mtaandika katiba, katiba itakuwa ni yenu.

Asanteni sana.

(Applause)

**Com Paul Wambua:** Changei tugul?

(Applause)

Kawaida wazee walisema, vijana hawasemi maneno mengi. Yale ambayo ni ya muhimu yamesemwa tayari na Commissioner Bibi Asiyo na Pastor Zablon Ayonga.

Kwa hivyo yangu nikuwasalimu kwanza na pili kuwashukuru kwa kufika maanake kama ilivyosemekana, nafasi ni hii tu. Tuliambia sisi kama tume, tutawapatia nyinyi nafasi mzumze na kwa kawaida tukianza kikao tunamaliza wakati mtu wa mwisho ameshazungumza. Kwa hivyo nafasi ni yenu, msije mkasema hapo baadaye ya kwamba sisi hatukupewa nafasi kuchangia katiba ilipokuwa inaundwa. Katiba ni yenu, na hii imeamuliwa iwe ni a people driven constitution, kwa hivyo kila mtu lazima apewe nafasi ataje angelipenda yawe kwa katiba.

Kwa hivyo ningependa kuwashukuru kwa kufika, ninafikiria na ninatarajia tutakuwa na siku njema na maoni ambayo yatatolewa hapa yatakuwa ni yale ambayo ni ya muhimu na yatachangia katiba nzuri. Kwa hivyo asanteni sana.

(Applause)

**Com. Abubakar Zein:** Habari ya asubuhi.

(Applause)

Nina furaha kubwa kuwa nanyi leo na nina shukuru kwamba nimepata fursa ya kuja kukutana na nyinyi. Na kama alivyosema mwenzangu baada ya wazee kuzungumza, ni ada desturi na mila zetu kuafiki na kukubali na kusema kwamba, tunayaunga mkono waliyoyasema wazee. Na kama alivyosema mwenzangu kwamba sisi tunafuraha kwamba mmefika na mmejitarisha kutoa maoni. Kwa hivyo kazi yetu itakuwa ni kupokea maoni hayo na kuyafanyanyia kazi na tunawahakikishia kwamba maoni hayo yatakuwa ni kati ya maoni ya wakenya wengine yatakayotumika kujenga katiba mpya.

Asanteni sana.

(Applause)

**Com. Pastor Ayonga:** Asante kwa hizo salamu zote ambazo zimetoka kwa Commissioners, sasa tunataka kuanza our serious

business. Na kabla hatujaanza, ningelipenda kusema haya machache kwa utangulizi.

Kwanza: Leo si siku ya maswali; mmekuja hapa hatutumaini kwamba mtakuja kutuuliza maswali kwamba mambo ni hivi na hivi, tunataka je, hapo tungefanya nini?

Kuna maswali yaliyofanyika wakati wa civic education, mambo ya maswali yalikwisha. Leo tumekuja tukitumaini...

Karibu Bwana Hosea, karibu, karibu sana.

Nilikuwa ninasema kwamba leo si siku ya kutuuliza maswali, leo ni siku ya maoni. Tuna tumainia kwamba umeshatayarisha maoni yako ulipokuwa nyumbani na umetaka kuchangia katiba ukisema hivi na vile ndivyo unavyotaka, siyo kutuambia kwamba mnataka muangalie. Sisi hatuungalii kitu, sisi tumekuja kukusanya maoni. Kwa hivyo kama ulikuwa unakuja kutuuliza maswali, badilisha mawazo yako.

Kitu kingine: Kuna kijitabu tulicho tumia watu ili kiwasaidie tu kuchangia mawazo yao, kiwe kama changa moto kwao kwa kufikiri juu ya sehemu mbali mbali ya katiba. Hapa leo hatukuja kama Mwalimu amekuja darasani amechukua text book na ana-expect wanafunzi kujibu juu ya waswali yaliyomo katika hiyo text book kwa maana nimeshaona pahali pengine mtu anakuja amebeba kile kijitabu chetu na anaanza kusema “namba moja: hii na hii na hii, jibu ni hivi na hivi”. Kama tungekuwa tunafanya namna hiyo, mtu mmoja tu ndiye angeongea hapa, ajibu hicho kitabu chetu, tuseme tumemaliza hizo namba na kurasa, turudi nyumbani.

Leo tumekuja mchangie mambo makubwa makubwa mazito mazito na ambayo unasema dhahiri, siyo yale ambayo unapita round kwamba ni hivyo na hautuambii unalolitaka tumetaka useme lile ambalo unalolisema.

Kingine: Hatutaki jina la mtu yeyote kutajwa hapa, jina la mtu. Kitu ambacho tunachangia ni issues, mambo yanayotendeka, mambo tunayo tarajia.

Tena, tutatumia time; mnaangalia, hall imejaa na sisi tunatazamia kila mmoja aliyomo hapa atakuja kutoa maoni. Kuna wengine kweli mmekuja kama observers, kusikiza. Tungependa kama umekuja kusikiza, uwe kimya. Hatutaki baraza zingine hapa, baraza ni moja tu na ni yule anayeongea. Na yule anayeongea aweza kusema vitu pengine wewe hupendi, hatutaki umkataa toka hapo ambako umekaa, ungojee wakati wako, hayo ni maoni yake. Tunataka maoni ya kila mmoja yaheshimiwe, uyapende, usiyapende, ni maoni yake na kila mtu ana uhuru wa kusema jinsi apendavyo.

Atakayeongoza kikao hiki asubuhi ya leo, nimemuuliza mama Bibi Asiyo aongoze kikundi hiki lakini kabla hajaanza, ningependa mum-recognize bwana Hosea Kiplagat ambaye ameingia. Bila shaka Bwana Hosea, tungependa kusikia umetukaribisha hapa kwako na utusalimu pia.



(Applause)

**Hosea Kiplagat:** Commissioner Ayonga na wenzake, mimi ningetaka tu niseme, nikiwa mmoja wa viongozi kutoka wilaya hii ya Baringo, mnakaribishwa.

Mimi nimekuja kama stakeholder wa district hii na ninafikiri wakati nitakapopewa nafasi, mimi pia nitazungumza yale niko nayo. Ninafikiri langu tu ni kusema asante sana kwa yale yote umetueleza. Thank you.

(Applause)

**Com. Pastor Ayonga:** Kwa sasa nitampa mama Asiyo nafasi ili atupe taratibu ni jinsi tutafuata ili tuweze kupatia kila mtu nafasi. Na unapoambiwa dakika ni hizi, tafadhali utii. Hatukuweka hizo dakika bure, ni kwa maana tunajua tusipokata hivyo, wengine watatoka hapa siku ya leo bila ya kusema kitu.

Mama Asiyo sasa nafasi ni yako na utuongoze kwa mkutano.

**Com. Hon. Asiyo:** Asante sana Pastor Ayonga kwa kunipa fursa hii ya kuendesha mkutano ambayo tunafanya hapa kwa kikao cha Kabarnet County Council. Na vile umesema, ninataka kuhimiza na kusema kwamba:

I now officially declare this meeting as an official sitting of the Commission to harvest the views of the people of this constituency and as the Act requires, you should feel very free because the Act protects you and gives you the right and the freedom to say what you think will help to improve our nation.

Tukianza kuongea, wale walio na memorandum watakuja hapa mbele, watapeana memorandum yao, ninataka kuwahakikishia ya kwamba hiyo memorandum umeandika itaingizwa kwa computer, hata comma yake itaingizwa kwa computer. Hakuna kitu umeandika itakuwa nje ya maandishi yetu ya computer kabla hatujaanza kufanya analysis, tukishasikiliza maoni ya watu wote wa Kenya.

Pili: Kuna watu ambao hawajaandika na wanataka kusema tu kwa midomo yao, tutawapatia dakika kama tano ikilingana na vile uwingi wa watu utakuwa. Pengine saa zile watu watakuwa wengi sana, tutapunguza muda lakini kwa wale wameandika, wafanye tu highlight ya yale mambo muhimu ambazo wanataka tusikilize kwa mdomo yao ilituweze pengine kuwauliza maswali kama kuna haja ya kuuliza swali lakini kama wameandika wajue yote yataenda na yatafika kwa maandhishi ya kitabu chetu kikubwa kule Nairobi.

Na kama umezungumza, kuna register pale. Utaandika jina lako na usione vibaya ukiulizwa maswali mengine pale kwa maana ni vizuri tukujue vizuri ili siku ingine na ni siku karibu, watu wa Kenya watachagua watu mia sita na kama hamsini hivi, wazee na vijana na kina mama, ambao watakutana mahali pengine hatujui itakuwa wapi, watasoma hiyo mambo mlisema na watajadilia

kabisa kwa hiyo ripoti yote. Ndiyo watakubaliana kwamba kwa kweli haya ni mambo watu wa Kenya walisema na hivi ndiyo tutafuata, katiba ya Kenya itakavyokuwa.

Kwa hivyo ni heri kusema vizuri, sauti isikike kwa machine yetu na pia ukiulizwa maswali hao uyajibu yote, ndiyo kama kutakuwa na shida siku hiyo tuko Kabarnet, tutakuja kukutafuta tukuweke chini tena, tuweke maandishi yetu halafu uongee useme kama ulisema kweli, au ni sisi ndio tulisema uwongo.

Na saa ile tukiongea leo, tukiona mtu mlemavu au mzee au mtu ambaye ni mgonjwa au mama mja mzito, tunaweza kumpa nafasi aongoe hata kama alikuja amechelewa. Mambo yale mtaongea nyinyi wenyewe mnajua. Ninajua pengine mtaongea juu ya mambo ya utaratibu wa serikali, vile mngpenda iwe kwa siku sijazo, mambo ya uongozi.

Mambo pengine ya watu walemavu, vile mnataka waishi kwa miaka ijayo kwa maana kwa kweli hawajapata nafasi nzuri miaka hiyo mingine iliyopita. Sasa kwa kikatipa muwapatie nafasi kamili ya kuishi kama watu wengine wa nchi hii.

Mambo ya watoto muangalie sana mtueleze, na elimu yao. Pengine mambo ya vijana, mambo ya wazee, mambo ya kina mama, mambo ya uchumi, mambo ya mashamba, kila kitu ile nyinyi wenyewe mnaona mnataka iingizwe kwa katiba hii mpya, mjione mko huru kabisa kuongea na sisi.

Nimeshukuru sana kwamba Bwana Hosea Kiplagat amepata nafasi ya kuja kukaa na sisi. Yeye ni kama mtoto yangu, mimenjua tangu zamani sana na ni mtu mwema sana. Na nimeona amefika, nimeshukuru sana. Na ninaona wazee pia wamekuja na ni heri tutii wazee. Unajua university kubwa sana ni ya uzee; mtu anasoma mambo wengi wakati anaishi dunia hii. Kwa hivyo msidharau mambo yanatoka kwa vinywa vya wazee, myasikilize kwa makini. Nao wazee mtusaidie, na muwasaidie vijana ili katiba yetu iwe nzuri.

Yule ambaye alikuja mapema sana na alijiandikisha kuwa anataka kuongea ni Mama Lydia Jeruto Toroitich. Yeye atafuatwa na William Kiprof halafu kama Bwana Hosea atatuambia wakati unataka kusema, tutampa nafasi aongee na kama kuna wazee wanataka kurudi mapema au wagonjwa pia tutawapa nafasi. Kuna Stephen Tomno ambaye pia ataongea na Zippora Komen pia amejiandikisha kama mtu anataka kuongea halafu atafuatwa na Alfred Kosgey na tutaendelea namna hiyo isipokuwa katikati... Msichana utakaa hapo chini vizuri, kitaratibu, useme kwa ufupi na useme ile mambo inakuhusu na itaingia kwa ile machine na sisi pia tutaandika vile unasema. Haya! Una nafasi sasa ya kuongea.

**Lydia Toroitich:** Quests of honour, ladies and gentle men, asante sana kwa kuja kwenu Kabarnet.

Ile Lydia Jeruto ninasema, ninaomba nirudishiwe kazi yangu ya casual hospitali. Na mimi ninaomba kama wagonjwa ni wagonjwa na unaambia enda ita daktari, wasiseme ni kazi ya out-patient, ya out-patient na kazi ya ward ni ya ward kwa sababu patient akiwa mgonjwa anakuja daktari wamuangalie.

Siku ingine mgonjwa wa Out-Patient alikuwa mgonjwa, mimi nikakimbilia watu wanaitwa ICU nikawaambia “Excuse me, kujeni muangalie huyu patient, huyu patient yuko mgonjwa” Wakakataa wakasema kazi ya out-patient ni ya out-patient na kazi ya ward ni ya ward. Ni vizuri kama daktari anaitwa aje asaidie patient, awasaidie kwa roho mzuri.

Asanteni.

(Applause)

Com. Hon. Asiyo: Asante sana kwa kuzungumza maoni yako, tutaona vile itatengenezwa. Asante.

**Com.Pastor Ayonga:** Ningalipenda tunapofuata hii list, kwamba kwanza tungewapa wakati watu ambao wanatoka Baringo Central yaani tumekuja leo kuwahudumia watu wa Baringo Central na kama kuna mtu mwingine ambaye ametoka kwingineko,tutampa nafasi baadaye. Ikiwa umejua umejiandikisha katika list hii, hakuna neno lakini kama wewe si mkaaji wa Baringo Central, tungelipenda ungetuambia sikutoka Baringo Central lakini nyumae tunaweza kukupatia nafasi. Tumeelewana?

Tumetaka tu kufanya haki. Kama nimekuja nyumba yako kukuhudumia, ninataka nijue kwamba hawa ndio watoto wako, kwanza niwahudumie ndipo wale wageni waliokutembelea pia nitawahudumia. Sisi tunahudumia kila mmoja kwa hivyo yeyote asione ubaya, na si ubaguzi lakini tunataka kufuata priorities. Thank you so much. Mama Asiyo unaweza kuendelea.

**Com. Hon. Asiyo:** Asante sana mzee Ayonga. Hata kwa sheria yetu inasema tutasikiliza maoni ya watu wa constituency, kila constituency. Kwa hivyo kama mtu ametoka nje ya area hii, aeleze kabla hajaongea na hataongea mbele ya wale watu wa hapa. Kwa sasa kuna Bwana William Kiprop ambaye amejiandikisha kuongea. Mzee Kiprop nenda hapo mbele ukae, uchukue machine, hiyo microphone, halafu uanze kuongea. Asante. Bwana Kiprop ukimaliza, Bwana Stephen Tomno atakufuata wewe, awe tayari pia.

**William Kiprop:** Bwana chairman wa Commission, neno langu ninalotaka kuandikisha ni kuhusu sheria inayohusika na mambo ya watoto: Watoto hawatii wazazi , watoto hawatii...

**Com. Hon. Asiyo:** Sema jina lako kwanza mzee.

**Mzee Kipruto:** Jina langu ni William K. Kiprop kutoka kipkaech sub-location, Central Baringo.

Kwa hivyo sheria ninavyotaja ni kuhusika na mambo ya watoto. Hawatii wazazi na mbeleni zamani wakati sisi wazee tulikuwa tukitii wazazi wetu na hata watu wakubwa wakubwa. Unakuta watu hawawezi kutii na hata sasa ukiona mtu hata hawezi kujua, kama councilor akipita hapa, ajulikani kwamba ni nani ama kama baba akipita huku, hauwezi kujua ni nani. Ukimzalimia mtoto anasema mising, mising na hiyo haikuwa kwa sheria yetu ya ki-Tugen.

Lazima mama aheshimiwe, baba aheshimiwe, mtoto aheshimu baba. Kwa wakati huu sasa tunaona hiyo imeharibika na unakuta

watoto wanaendesha mambo ya pombe, watoto wadogo wanaharibika na mbeleni watoto hawakuwa wanakunywa pombe. Hata kina mama unakuta hawakuwa wakinywa pombe lakini wakati huu sasa imechafuka.

Kwa hivyo sheria ninataka iwe kama ile yetu ya zamani, kuweko na amri kali na kulikuweko hata kiboko. Watu wanawatandika watoto wakicheza cheza wanachapwa na kwa hivyo ingefaa hiyo sheria ipitishwe iwe kama zetu. Sisi tulichapwa na tungali tuko, mbeleni tulikuwa tukichapwa na tungali tuko na nguvu na tumefuata sheria.

Unakuta mtu hata akiingia kwa ofisi ya DO, watu wanaingia tu hivi hivi, hawawezi kujua DO ni nani, haya! Ukiwakuta wanaingia kwa chief, wanaingia tu kiholela, hawawezi kumheshimu kama ni chief.

Kwa hivyo tunataka sheria iangaliwe kwa upande huo, lazima waheshimiwe. Mpitishe sheria iheshimiwe watu wazima na watu wote.

Second: Kuhusika tena na mambo ya ardhi. Ardhi katika sehemu yetu hapa imeharibiwa na vijana. Mzee anasema hii ardhi tunagawanya na fulani na fulani, mpaka ilikuwa inapita sasa kijana anakuja kuniingilia akisema mzee si mpaka yetu inapita huko.

Kwa hivyo lazima mpaka ifike huko na lazimisha mimi niseme uwongo kwa sababu yeye anataka hii ardhi iwe yetu na hiyo si haki.

Kwa hivyo vijana ndio wameingilia wazazi na wazee. Kwa hivyo ninataka hiyo sheria ichuguliwe kabisa kwa mambo ya ardhi, hasa ardhi kwa sehemu yetu ya Baringo, hapa hapa, ardhi hapana iko mzuri. Ni hayo tu niliyokuwa nayo.

**Question:** (Inaudible)

**Mzee Kiprop:** Tungependa ardhi, wako wazee wa zamani, wazee wawe wakichunguza mambo ya ardhi. Wazee, hapana husika na vijana. Kwa hivyo nimemaliza hapo.

**Com. Pastor Ayonga:** Mzee jambo la ardhi linakuwa na maana kubwa sana katika katiba yetu na ningelipenda mzee utuambie, hawa vijana ambao umeongea juu yake, vijana pia wanataka warithi ardhi. Je ungeweza kutupa mwelekeo, hii ardhi ingalifanywa namna gani.

**Mzee Kiprop:** Kwanza kuhusika na mambo ya ardhi, mzee na wale wengine walio pamoja, wazee, wajue hii ardhi tulikuwa tumefyeka zamani tulikuwa hapa, mpaka wa huyu ni hapa, mpaka wa huyu ni hapa na iwe under mzee halafu mzee wakati wake atapeana kwa mtoto yaani kurithi. Watoto watagawiwa, kama ni mbili au tatu, wanagawiwa kwa kurithi. Si mtoto aje kuniambia ati nisongeze ya huyu kando huku na turudi tusongeze ya huyu ili shamba yetu ipanuke bila kutii mila yetu.

Kikwetu, mtu kunyakuwa shamba ya wengine ni mbaya, ni dhambi.

**Com. Pastor Ayonga:** Na tena ardhi hii mara nyingi tunaposema kwa watoto, tunafikiria watoto wa kiume. Je, una wazo lolote kuhusu watoto wasichana?

**Mzee Kiprop:** Kulingana na kimila yetu.... (gap cos of end of side A)

Kama hakuolewa na mtu, basi ni lazima apewe shamba nyumbani, ataenda wapi.

(Applause)

Na kama yule ameolewa, ameenda kwa nyumba yake, hawezi taka shamba yangu tena ati kurithi shamba

(A bigger round of Applause)

**Com. Zablon Ayonga:** Hebu niwaambie kitu kimoja. Katika recording yetu, tusingalipenda kuruhusu makofi kwa maana we are not holding a political rally. Tafadhali tungelipenda mheshimu. Hapa tuko kama watu waluo kotini na kule kotini hata kama mtu amesema ushahidi mzuri wa namna gani, hakupigwi makofi. Kwa hivyo tumetaka kufafanua juu ya tofauti hizo. Asante mzee kwa maoni yako. Wengine pia watatoa yao.

**Mzee Kiprop:** Thank you very much sir.

**Com. Hon. Asiyu:** Asante Bwana Kiprop. Sasa tuko na Stephen Tomno na atafuatwa na Zipporah Komen. Zipporah Komen uwe tayari na wewe utafuatwa na Kipyegon. Endelea mzee.

**Stephen Tomno:** Commissioners, ningetaka kushukuru kwa nafasi hii nimepata. Ningetaka kuzungumza juu ya mambo manne.

Ya kwanza ni juu ya government structure, ya pili ni mambo ya urithi ama inheritance, ya tatu ni juu ya nidhamu ama elimu ya watoto wetu na ya nne ni juu ya sheria ya machiefs.

**Com.Hon. Asiyu:** Ningetaka kusema kama kuna mtu anataka kuongea ki-Tugen, tuko na mtu ambaye atatafsiri kwa kizungu au kiswahili, kwa hivyo unaweza kusema lugha yoyote na ni heri umeanza na kiswahili, endelea namna hiyo ni mzuri.

**Stephen Tomno:** Asante. Kwa mambo ya government structure tumekuwa na President

**Com.?:** Tafadhali sema jina lako.

**Stephen Tomno:** Mimi ninaitwa Stephen Tomno kutoka Orokwo Location. Ningetaka kuzungumza juu ya election ya President: Tumekuwa na Presidents wawili na tunasikia President aliye sasa atastaafu na hatujui yule atakuja kushika usukani atakuwa namna gani. Maoni yangu ni hii, ya kwamba President ambaye ataingia, tungetaka awe ni President ambaye ni Ceremonial President.

Na huyu Ceremonial President awe ni mtu tunaita kwa lugha ya kimombo Nationalist; mtu ambaye hatakuwa akiangalia kabila yake ama dini yake, ni mtu ambaye atakuwa akipenda kila mtu katika Kenya.

Ninafikiri nimemaliza kazi ya President na departments zingine za serikali itakuwa kama vile ilivyo isipokuwa nikisema Ceremonial President, inaonekana hiyo powers ambayo president amekuwa nayo kwa miaka mingi itakuwa imeletwa chini kidogo.

Sasa ninaingia kwa ofisi ya Prime Minister: Ningetaka kutoa maoni yangu ya kwamba yule ambaye ningependelea sana aendelee na kazi ya kushikilia kazi ya serikali, awe Prime Minister, ambaye party yake itakuwa na majority ya members of Parliament, na election ya members of parliament iendelee kwa miaka mitano. Ikiwa party yake itaendelea kupata kura kwa wingi, naye aendelee awe Prime Minister ama mwingine kutoka hiyo party anaweza kuwa Prime Minister.

Na kama party ingine ikipata majority ya members of parliament, wanaweza kutoa Prime Minister.

Ninaenda ya tatu: Ningependa kusema ya kwamba tuwe na federal government. Kwa sababu gani nimetoa hiyo? Kwa sababu kumekuwako na exploitation ama unyanganyi kutoka makabila ambao wamepata education ya zamani, wanaingilia makabila ambayo hawana education, wanawanyang'anya mashamba, wananyanganya mali, wananyanga'ya hata plots na kila kitu.

Kwa hivyo tukiwa na federal government, ninafikiri hapo kazi ya kuchunga kila mmoja katika area hiyo ndiyo itakuwa mzuri. Tumeona ya kwamba hawa watu watu ambao wanatoka mahali pengine, pengine wanatoka province ingine mpaka province ingine, ikiwa wanataka kupata accommodation kama vile tulikuwa tunafanya zamani, kama Mtugen anatoka hapa anaenda Nandi, lazima afanye mambo ya wanandi na asijiite ama alete desturi yake ya Tugen aende huko Nandi halafu ajiite yeye ni Mtugen. Hiyo ni mbaya sana. Ama Mtugen akienda huko Maasai land awe ni mtu ambaye anaheshimu watu wa Maasai na sheria ya Maasai.

Tukifanya hivyo, kila kitu itakuwa mzuri na hakutakuwa na mambo ya kuchocheana ama mambo ya vita mahali popote.

Nikisema hivyo, kama kuna watu ambao wametoka mahali pengine tuseme kama wametoka Nyanza ama pengine Western ama pengine North Eastern, kama wamekuja Rift Valley wakiwa wamekuwa elected, ningetaka wa-identify themselves with the people of that area. Yaani awe mtu ambaye anaona wale watu wa upande huo kama ni watu wake na kazi yote awafanyie wale watu wa huko.

**Com. Hon. Asiyo:** Ninaona wakati wako unaenda ukiisha, kama una mambo muhimu haujataja ungetaja sasa maana hiyo karatasi yako sasa ni mali yetu, tutachukua na tutaweka kwa computer yetu. Sasa huwezi kurudi nayo isipokuwa ukitaka kwenda kuandika vizuri na kuleta.

**Stephen Tomno:** Nitaenda kuandika vizuri halafu nirudishe.

Sasa uchaguzi wa councilors: Ningetaka kuchangia ya kwamba election ya councilors kwa sababu ya communication na mis-communication wawe watu wa elimu na ikiwezekena wawe form fours na kwenda mbele.

Sasa ninaingia kwa mambo ya urithi: Ningetaka kusema vijana ama boys na wasichana wana haki ya kupata elimu sawa kutoka kwa wazazi wao. Masomo yoyote hata kama ni kuingia university na wapi, hiyo iwe right ya kila mtoto katika familia.

Na mambo ya ardhi: Ningetaka kusema kwa desturi yetu msichana huwa hawezi kupatiwa ardhi nyumbani na kuna sababu ambayo nitaenda kusema; tunasema ya kwamba msichana anapatiwa ardhi mahali ambako ameenda kuolewa. Na msichana ambaye ameolewa na kijana wa hiyo nyumba, tunasema anapata ardhi yake kwa hiyo nyumba ambaye amekuja kuolewa. Sasa atakuwa mtu wa hiyo nyumba na atakuwa na equal rights kutoka kwa baba ama mama wa hiyo nyumba.

Kwa hivyo sababu yetu ya kusema hivi ni hii; tukikubali watoto wavulana na wasichana kukaa kwa kiwanja moja, kutakuwako na shida siku sijazo. Watoto wataanza kuoana, halafu baadaye ndiyo tutapata shida kubwa sana, ambayo ungepata watoto ambao pengine akili zao haziko timamu. Wengine hata wanaweza kuzaliwa watoto wa mguu moja ama mkono moja ama wenye wanakosa hata macho.

**Com. Hon. Asiyo:** Hapo tumeelewa maana umeandika. Sema jambo moja ya mwisho ya muhimu ambayo ungetaka tusikilize maana maandishi yote itafika kwetu.

**Stephen Tomno:** Asante. Pengine wazazi wangetaka kupatia msichana haki ya kupata shamba, pengine huyo msichana amekuwa mtu mzuri kwa nyumba hiyo na tunasema ikiwa mzazi fulani ama wazazi wawili wanataka kumpatia msichana shamba, isiwe hapo karibu. Wanunuliwe shamba mbali na nyumbani ili wa-avoid hiyo mambo. Thanks.

**Com. Hon. Asiyo:** Umemaliza? Kuna swali moja hapa.

**Com. Paul Wambua:** Umetaja kuwe na Ceremonial President lakini kitu kimoja tungelitaka kujua ni kama huyo Ceremonial President atakuwa na kipindi kimepimwa awe akitumika baada ya kimoja ama vipindi viwili hawezi kuendelea na pia kama akifika umri gani pengine astaafu, tungetaka kusikia maoni yako kuhusu mambo kama haya.

**Stephen Tomno:** Ningetaka kuongeza ya kwamba President ambaye ni ceremonial awe elected baada ya miaka mitano na election yake ionekane ya kwamba isifanywe pamoja na ya wabunge. Yake itaingia pekee yake halafu baada ya hiyo yeye

mwenyewe sasa atakuwa na nafasi na nguvu ya kuendesha kazi ya hao wengine.

**Com. Hon. Asiyu:** Tunafahamu hiyo lakini hata mimi nina swali moja tu ya mwisho. Kama mzee huyu unaongea habari yake amezaa wasichana pekee yake, wasichana tu, hakuna mwanaume, na pengine kuna wasichana wake wengine hawajakuwa na bahati ya kuolewa. Hiyo shamba yake itagawiwa watu wengine waende naye au hata hawa watoto wake alizaa hapo wanaweza kwenda kulima hapo na kupata chakula?

**Stephen Tomno:** Kitu ambayo tulikuwa tunafanya zamani, kama mzee ama mama wa mzee fulani hakuwahi kupata kijana, ile shamba wanaweza kuuzia watu wa jamii yao halafu hiyo pesa wanaweza kununua shamba kutoka mahali pengine. Maana hata jamii ya hiyo wangali damu moja. Kwa hivyo hata wakiolewa kutoka kwa family hiyo, hata naye ataendesha hiyo damu tena.

**Com. Hon. Asiyu:** Kwa hivyo wasichana hawawezi kupata nafasi ya kurudi kuona hata nyumba ya baba yao, waonyeshe wajuukuu hapa ndio babu alikuwa anaishi kwa maana sheria inakataa.

**Stephen Tomno:** Kwa Tugen ilikuwa inakataa. Basi niendele.

**Com. Pastor Ayonga:** Hapana.

**Stephen Tomno:** Imekwisha?

**Com. Pastor Ayonga:** Ilikuwa imekwisha.

**Com. Hon. Asiyu:** Sasa hiyo karatasi ni yetu, kama hukutosheka na maandishi, nenda rekebisha halafu utuletee. Maoni yako yote yako pale ndani tutachukua tafadhali. Asante sana Bwana Tomno. Mama Zipporah Komen kwa niaba ya Baringo Association for Deaf People. Tafadhali kaa pale mama Zipporah Komen. Or you have already got a written memorandum? Zipporah what you do, just mention the very... just highlight important issues because we have this with us already and you don't need to read it please.

**Zipporah Komen:** Ladies and Gentlemen hear am presenting for the Deaf Association people in Baringo. I am sorry, the time if I have to sign for the deaf will have to be long because if I don't sign it is a problem.

I don't know, even in school the deaf people are given a lot of years to study and finish their work but if given little time to maybe sign for them, it is a problem. I don't know, if you can allow me to read some, the better.

The deaf people should be allowed to own driving licences and hence just the same as other countries. By the way the deaf are



hear in front. May all the deaf stand. I am representing them and may be when you see them just the way they are seated there you think they are people who are hearing but they are deaf.

The media should have interpreters, so that they follow current affairs like other hearing friends. This will help them understand national and international news.

Equal distribution of resources and other things to the deaf: The deaf should be given a percentage in Jua Kali kiosks and in the market stalls, in education and in civic and parliamentary seats and also in work places or employment.

Funds to be set aside to give to the deaf to start their own work, business so that they can be independent.

Protection against discrimination in land allocation, education by the government and parents.

The first five are mostly about the deaf but as I go to the sixth one it is about the nation.

Retain the concept of nominated MPs.

Anybody who has tried to vie for parliamentary that year should not be nominated for it is an abuse to the electorate.

People of high integrity should be elected.

Special measures to be put in place to increase women participation in parliament.

Borrow a leaf from Uganda, women to be elected by co-women from given regions.

A president to be removed from office whenever there is misuse of power, for example corruption or entertaining corruptive figures and misuse of public funds.

There must be an interpreter in court whenever a deaf person is being charged.

Mayors and Chairmen of county councils to be elected by people for left alone they buy people hence we get people who don't deserve to be in that post.

People to have rights to recall their councilors. This should be done by the committee members at a ward and report and report to the county councils.

Remuneration of councilors to be determined by the ministry of local government or the resources in that district.

Reserve seats for the deaf, blind and the physically disabled people.

The election process should be simplified: About this, I have three points to register;

Be registering throughout the year, votes and counting of the votes be done in the stations where voting was done, computerize every constituency returning office.

Electoral Commissioners should be holding degrees and must have served diligently before in other offices.

Appointment of Electoral Commissioners should be in parliament and each region to be represented.

The Electoral Commission Chairman should enjoy security of tenure for tax money is limited to cover all the Commissioners.

There should be two terms of five years each in office.

The interests of people with disability is not fully taken care of, for the physically handicapped can not climb on buildings.

There are no driving licences for the deaf, no identification cards by the nation for the deaf and respect for the blind and the physically handicapped when crossing roads.

The constitution should address the disability of the hearing impaired, the blind or the visually impaired, the mentally and the physically handicapped.

The constitution should guarantee and protect of the children in education especially the early childhood education.

In this nation, nursery school teachers are not employed by the government yet this is the foundation of human beings.

Child abuse by parents and teachers and other people should be dealt with with a lot of seriousness.

**Com. Hon. Asiyo:** Zipporah we have all these that you are reading listed in this memorandum and ---- (Inaudible) and you have just one minute now to round up and ----(Inaudible).

**Zipporah Komen:** Okay. I think there are about five points remaining, I will just rush through.

The mechanism which parliament should control the management of public funds is to have a strong anti-corruption unit but not the use of the police for they are the most corrupt people in this country.

Attract competent Kenyans to work in public offices by paying them very good salaries and allowances.

Anybody with a bad record should not hold a public office.

Public officers should declare their assets anytime they are required to do so.

**Com. Hon. Asiyo:** Yes. Now the time is absolutely over, if you can please round it up now. We have your document and nothing will be left out of it.

**Zipporah Komen:** Okay. Thank you.

As a teacher, this part of corporal punishment should continue. If you spare the rod, you will spoil the child. Please this one is an important and maybe the last point to tell you. Thank you very much.

**Com. Hon. Asiyo:** Thank you very much. Please, just a minute, there is a question.

**Com. Pastor Ayonga:** Zipporah you have said Electoral Commissioners should be degree holders. What do you think we can gain from degree holders and what problems have we undergone with the present Electoral Commissioners? Is it because if we had any problem it is because there was no degree person? Is there a magic that the degrees could do to make our Electoral Commissioners or system become more efficient?

**Zipporah Komen:** Thank you sir. I think when we elect people with education to such offices, at least education is a right, at least you know what you are doing but not to be told. You see if you are not educated, you may just give views because other people are giving you but if you are really educated, you will give views because you feel the views will help the people.

**Com. Pastor Ayonga:** Education does not mean a degree. Education has got you know lots of ways of having education. All of us who have come here today to give the views, and people are giving very responsible views. They don't need to have a degree and to be educated is not in the book work alone. Bookwork, yes, is one aspect of education but there are other things also that we should include and let's we not think that an educated person is a person with a degree. You are limiting other people who can also contribute.

**Zipporah Komen:** Sir, I don't know whether...

**Com. Wambua:** Let me put it this way. Are there other people who should have limitation of education because you have only specifically referred to Electoral Commissioners and in one of those questions we have asked in the booklets is that is should there be education limit for councilors, for presidential candidates, for MPs; you have specifically referred to the Electoral Commissioners and left out all this others.

Can we have a comment on each of these?

**Zipporah Komen:** Well, you have asked though I went through all those questions, they are in this book but when it comes to... may you really want to know my views when I come to this of councillors. About the Electoral Commission, that is an office where the people who are holding it should really know what they are doing but be a councilor, the knowledge you have acquired can assist you.

I don't want to say a councilor should be a degree holder or a form four holder but if he is really capable of leading the people in that ward, then there is no reason why he should not be elected.

**Com. Hon. Asiyu:** Thank you very much. Just a point of information Zipporah, the government has already put in place that for all future elections, the votes will be counted at the polling station.

**Zipporah Komen:** Thank you very much.

**Com. Hon. Asiyu:** Thank you very much. Can we now have Mr. Alfred Kosgey? If Mr. Alfred Kosgey has not come, then we will ask Joel Kipkoech. Is he here? Kama Joel hayuko na pia Alfred Kosgei hajafika, tuko na Elizabeth Chesire. Mama Elizabeth Chesire, halafu atafuatwa na Kibichii Chebii lakini saa ile Alfred Kosgey anakuja, tafadhali atakuja hapa mbele. Wewe ni nani mzee? Joel Kipkoech. Okay. Wewe utaongea mbele ya mama Elizabeth Chesire. Nilikuwa na ikawa hujalingia lakini kwa vile sasa umeingia, kaa chini pale.

Mama utangojea kidogo huyu Mzee Joel aongee halafu utafuata yeye lakini ukae karibu ni mzuri. Alfred Kosgey hayuko na huyu ni Joel Kipkoech ambaye pia ataongea bila maandishi na tutampa nafasi atueleze juu ya katiba mpya. Unaweza kuendelea sasa mzee.

**Joel Kipkoech:** Mimi ni Joel Kipkoech kutoka Central Baringo. Kwa maoni yangu ningeomba serikali yetu, mimi ninaongea juu ya forest, katika forest hii ambayo iliwekwa na wazee wa kale, ningefurahia hiyo sehemu itengwe na kama kutakuwako na maneno kwa sababu tumeona vijana wengi wa siku hizi hawajali hiyo sehemu na kwa upande ya wazee, wanajua hiyo sehemu ya forest kun dawa, inaleta mvua, inaleta hata wakati wa kiangazi kuna matawi ambayo wanyama wanaweza kula.

Kwa hivyo mimi ninauliza serikali yetu hiyo sehemu ilindwe na isiharibiwe kwa sababu ikiharibiwa, hata upande ya chemchemi ya maji...

Nowdays nikitazama kabisa hiyo forest, vijana wameenda bega kwa bega kutafuta kuni, kutafuta namna ya kuuza ili wapate pesa, kwa sababu ya ukosefu wa kazi, lakini hiyo sehemu itakuja kuharibika wakati ujao, let us say ten years to come, itakuwa bure. Sehemu ya maji haitakuwa, dawa haitakuwa hata matawi imekwisha yote na tutakosa hata mvua.

Ya pili mimi ninaongea juu ya mashamba kijijini humu, kwetu nyumbani: Zamani za kale vijana hawangeweza kuongea hiyo sehemu ya mashamba kwa sababu kwa upande wetu wazee waliwekwa hiyo sehemu ya mashamba.

Ardhi ni kali, ni kitu muhimu kwa sababu Mungu aliumba hiyo ardhi na ikawekwa kama si kitu ya kuchezeza na watoto. Ni wazee tu. Kama kuna maneno, wazee wanakwenda kaa chini na kuelewa hiyo sehemu ya ardhi ni ya nani, ndiyo sasa itakwenda bara bara. Lakini vijana wa siku hizi wengi wao wanatumia pesa ili kupata kuharibu hata yule asiyekuwa nazo.

Kwa hivyo mimi ningeomba serikali yetu hiyo iwekwe chini ya wazee. Maneno yangu inatosha hapo, sina mengi kwa sababu mimi sikupata kusoma hayo masharta ya vile mtu angetakikana kuongea lakini mnaweza kunisamehe hapo.

**Com. Hon. Asiyo:** Asante sana, asante sana Mzee Joel. Sasa tutamsikiliza mama Elizabeth halafu nyuma ya mama Elizabeth, tutamuita Bwana Philip Cheptingu ambaye ametoka Moi University, Faculty of Medicine.

**Elizabeth Chesire:** Mimi ni mama Elizabeth Isaya Chesire wa kanisa la AIC Kapropita, Baringo Central.

Na mimi ninataka kusema habari ya watoto mayatima kwa maana nimeona wale watoto maskini, wale watoto mayatima, hata wale maskini, ninaona wako na shida sana na mimi ninaomba serikali yetu tukufu kutafuta njia ya kuwasaidia hawa watoto.

Zamani mababu zetu walikuwa wakiwasaidia sana watu maskini, lakini siku hizi ninaona watu wamekuwa tofauti. Watu walio na mali wanajipenda wenyewe, wanapendana wenyewe na kusaidiana lakini maskini hasaidiwi sana, hana usaidizi.

Na ingawa serikali yetu kama huyu Rais wetu, mtukufu Rais, kila wakati anasaidia watu wale hawana vitu kwa mashule, kuwapatia pesa. Halafu baadaye wakati hiyo pesa imeshaingia kwa mikono ya watu wetu wakubwa, hizo pesa zinaanza kupotea, wale walikuwa maskini kabisa hawapewi hizo pesa.

Sijui ni kutojua kuchunguza, viongozi hawajui kuchunguza au ni nini? Kwa maana ninaona maskini bado wangali tu namna ile ile na sisi tulisanya pesa mingi.

Ninaomba hiyo kwa unyenyekevu katiba yetu hii itazame sana.

Kama imeshasemwa hii ni ya wasiojiweza, wafanyiwe tafadhali. Hata ukisoma kwa Biblia, kwa neno la Mungu, inasema mlio na uwezo, bebeni nguvu ya wale hawana nguvu. Hilo neno liko kitabu cha Warumi 16.

Hilo ni langu la kwanza.

Neno la pili: Ninataka kusema habari ya wale wasichana wetu: Unajua siku hizi na zamani ni tofauti. Watu wamekwisha ongeseka sana. Zamani tulikuwa wachache, kwa kufundisha, walikuwa ni wachache lakini sasa watu wamezaa na wamezaa na

wamezaa .

Mimi nimezaa wasichana tisa, na hao wasichana tisa kama hawataolewa, wataishi kwa shamba gani? Lakini kitu ninachotaka hapo kwa wasichana, wasichana wale hawajaolewa, tafadhali baba awape shamba, mahali pa kuishi.

Lakini kitu ninataka kusema tena hapo, wasichana, ninataka amri iwekwe kwa katiba yetu kuwa saa hii watu wazae watoto wawili na watoshe. Kwa maana hakuna mahali pa kuishi. Watu wengi namna hii wataishi wapi?

Mimi ninahimiza hiyo, mimi ninasema sana hilo neno; ni vizuri kukataza hawa kuzaa watoto wengi sababu hawana mahali, hawana bwana na hawana mali. Hiyo ni vizuri katiba yetu iangalie hilo neno sana hata ingawa mimi sikuandika kitu kama watu wengine wanaopeana makaratasi yao. Mimi sijasoma lakini ninamshukuru Mungu wangu kwa maana amenifungulia ya kujua kusoma Biblia tu.

(Laughter)

Mimi ni mama ameokoka.

**Mr. Chesumei:** By selling the ideologies and policies to the wananchi.

**Com. Paul Wambua:** Okay. Sawa sawa.

**Mr. Chesumei:** Not coming and saying this is an ---? This person is bad, they should sell their good part of it. Any party, let us say DP or KANU should say these are our policies, we are going to do ABCD and they they go to the public and say this is what we are going to do.

**Com. Paul Wambua:** In short we need party discipline? Good. Any other point Bwana....

**Mr. Chesumei:** For that much I wish to thank you for giving me this opportunity.

**Com. Paul Wambua:** Okay, asante sana. Jiandikishe hapo. Next. What is your name?

**William Chelelgo:** Kwa jina ninaitwa William Chelelgo.

**Com. Paul Wambua:** William Chelelgo?

**Mr. Chelelgo:** William Chelelgo.

**Com. Paul Wambua:** Haya! Endelea Mzee.

**Mr. Chelelgo:** Asante Bwana Commissioner. Yangu ni machache.

Kwanza, Bwana Commissioner, sisi Tugen, tunaishi kulingana na jamii na jamii hizo tangu zamani walikuwa wanaishi sehemu zao nakuna mpaka zao. Wakati huo kuna watu ambao, mtu anaweza kwenda kuomba hifadhi kwa jamii fulani, anapewa hifadhi. Anaishi huko, anazaa huko mpaka watoto wao wanakuwa wakubwa. Wanaweza kurudi kwa plot yao nyumbani ama wanaweza kununua shamba mahali hapa, tangu juzi juzi wakati ilisemekana shamba inauzwa kwa sababu zamani shamba haikuwa inauzwa.

Basi, sasa yangu bwana Commissioner, ninapendekeza kuwa mipaka ya jamii ijulikane katika Katiba ili mashamba ya jamii yasinakuliwe na wengine kwa akili yao ama nini.

Ili kama mtu anaishi kwa jamii fulani ama amenunua shamba mahali fulani ama kipewa shamba fulani, akae na hiyo shamba yake, hana shamba lingine ambaye anaweza kushtaki jamii ati tunang'ang'ania shamba na yeye.

**Com. Paul Wambua:** Hiyo tumesikia.

**Mr. Chelelgo:** Kwa hivyo, hiyo ni yangu Bwana Mheshimiwa.

**Com. Paul Wambua:** Hakuna nyingine.

**Mr. Chelelgo:** Hakuna nyingine.

**Com. Paul Wambua:** Haya! Asante sana. Wachacha tumwite mtu wa mwisho hapo.

**Omulama Ayaya:** Asante sana Commissioners. Mimi ninaitwa Omulama Ayaya na niko na mapendekezo ambayo ningependa kuchangia Kuhusiana na hii tume ya marekebisho ya Katiba.

Kwanza kabisa nikigusia mambo ya kisiasa, watu wengi sana wamependekeza kwamba term ya President iwe terms mbili ya miaka tano tano lakini mimi ningependa kupendekeza tofauti kidogo kwamba kwa vile sasa Tume ya marekebisho ya Katiba huenda ikatilia mkazo njia ambazo zitafanya serikali, tuseme mikono tatu ya serikali kama tuseme legislature na Executive na Judiciary ku function sawa sawa, ikiwa hivyo, hata ikiwa President atakuwa na nguvu gani, ikiwa hata atakaa kwa ofisi mpaka akufie huko ama hata mpaka kura imtoe huko, kuna uwezekano kwamba anaweza kufanya hiyo kazi bila ku-abuse, kutumia mamlaka yake vibaya.

Sasa nilikiwa nataka kupendekeza Rais wa nchi awe anaweza kutolewa kwa kazi na kura ama kama ataweza kuchaguliwa na kuchaguliwa na kuchaguliwa, aendelee mpaka afe.

Ningetaka kupendekeza upande ya wajumbe kwamba MPs ndiyo ningependekeza kwamba wao wawe wakichaguliwa kwa kipindi kimoja tu ya miaka tano na kama angependa kurudia kuwa mjumbe tena, huyo yeye akae miaka ingine ishirini ndio tena aweze kusimama tena akitaka kuwa mjumbe. Otherwise wewe ukitaka kuwa MP, ukishafanya kazi yako kwa miaka mitano, unatoka kabisa, kijana mwingine anachaguliwa.

Tena nilikuwa nataka kupendekeza kwamba MPs wawe kati ya miaka ishirini na moja na hamsini.

Watu hawa wengine wawe wanaweza kuendea kazi kama ya ukansela ambayo hiyo ningependekeza isiwe na kipimo ya miaka wala masomo kulingana na vile mapendekezo ingine ilikuwa.

Pia nilikuwa nataka kupendekeza ya kwamba Katiba ile mtakuja nayo iwe inatetea pia the fear of God.

Kuwe kwamba kama Katiba ile ya zamani inasema kwamba Kenya is a Sovereign State. Pengune hapo tuongezee kwamba ni



sovereign state ambayo inatawaliwa na kuogopa Mungu; watu wawe wanaweza kumuogopa Mungu na tena hiyo katiba iwe inaweza ku-borrow heavily kutoka kwa Bible wakati inaandikwa.

Pili: Nilikuwa nataka kupendekeza ya kwamba kila juhudi ifanywe kuhakikisha kwamba Macommissioners hawafanyi hii mambo ya Katiba kuwa tu mambo ya hivi hivi kwa kuwachilia mambo ya kihivi hivi kupenyeza ndani kwa sababu kuna mambo mengi hata nikisikiza redio wakati mnachangia nasikiaanga sauti zenu kwa redio, watu wanapendekeza vitu zingine ambavyo zinaweza kushughulikiwa na wakati ama hata sheria ya asili ya watu.

Kwa mfano wakati watu wengi wanachangia mambo ya equity na equality na mambo ya roles kati ya wanaume na wanawake, kuna kuja hapo na kunakuwa na kuchanganyikiwa kwingi. Ndiyo nilikuwa napendekeza kwamba kama mnaweza kutumia neno la Mungu kidogo kuandika hapo, pengine mtaweza kupata jawabu haraka.

Kwa mfano mambo ya shamba, biblia iko wazi wazi sana kwamba ikiwa mtu akuzaa mtoto mwanamume, ile kitu inatajikana na shamba lake, assume that you we using the Bible but if you were using the tradition, say the Tugen tradition, you will also find that vile kulikuwa na mtu amependekeza hapa, kuna mtoto ambaye pengine hajaoleka na ni msichana na baba yake hakuwa na mtoto mvulana, vile hiyo shamba yao ingefanywa, so that we don't have a mix up and clashes of ideas and cultures.

Nilikuwa pia nataka kusema ya kwamba Katiba hii mtaandika iwe inaweza kuweka ndani measures za ku-stamp out laziness kwa maana shida zetu mingi, ikiniuliza mimi, ninaona zinaanza na uzembe so much so that tumezoea sana mambo ya kuomba omba na vitu ya bure na hiyo mambo inafanya, tuseme, wazee wengi wanategemea wamama ati waende wauze mboga pale sokoni waje wawalishe ama kama mtu anafanya kazi, anakunywa pesa yake yote, anawachia ati bibi ndiye atanunua chakula. Mtu kama huyo, mwanamume wa aina hiyo, inatajikana kuwe kunawezekana kuwe na kifungo hata kama ni ya miaka tatu ama hata kama ni ya nje, ya kufunga mtu kama huyo, ili ajifunze kutoa jasho ndiyo aweze kulisha family yake.

Mwisho nilikuwa kuomba hii tume, itakapopendekeza mapendekezo yake, ipendekeze kitu kuhusiana na mavazi ili kwamba kusiwe tu na free style of dressing so that kuna watu wanatutembelea uchi dunia hii. Ukienda Nairobi siku hizi kuna aibu nyingi sana ile tunaona huko so that kwa mfano kama ni mambo ya wanaume kufaa tight jeans kwa mfano, ijulikane ni wanaume wa miaka ngapi, kutokea miaka ngapi.

Ningependekeza wawe vijana kuvaa mambo ya tu-jeans na kuvaa tu-T-shirt na kuvaa kutembea na vifua nje.

Vile vile ningependekeza kama ni mambo ya kuvaa mini skirt, ijulikane ni watoto wa kiasi gani, ningependekeza wawe vijana miaka fulani, may be upto eighteen, mtoto msichana msichana kuvaa vitu kama mini skirt ama skin tight ama mambo ya malong'i haya mmezoea kuvalisha watoto wetu ili kwamba shida ya kijamii kama hii mtu alikuwa amechangia hapa ya rape ipunguke kwa sababu mahali kama South Africa, rape cases ziko juu sana kwa sababu mavazi ya huko hata mkiona kwa TV kwa vipindi ambavyo vinatoka upande huo, watu wanatembea uchi tu.

Sasa kama mtu anaweza vaa vizuri...

**Com. Paul Wambua:** Tumeshika. Kuwa na proper dressing code.

**Mr. Ayaya:** Yes.

**Com. Paul Wambua:** Kuna jambo lingine Bwana, ama hilo ndili la mwisho?

**Mr. Ayaya:** La mwisho kabisa, hilo pendekezo la Prime Minister hiyo, nilikuwa ninataka kusema kwamba haina haja kwa sababu kama Constitution yetu itaambatana na government ya Mungu, assuming that we shall borrow heavily from the Bible, then what it will mean is that, you see God is very overall; we don't have a Prime Minister in Gods government, may be we have ministers in form of Michael and Gabriel but we don't have those things of Prime Ministers and so on, those Corruptive posts that people are trying to create so as to get food. I do not know whether you are getting what I am saying.

**Com. Paul Wambua:** Oh yes. We have understood and it has been recorded.

**Mr. Ayaya:** Please, thank you.

**Com. Paul Wambua:** Okay, asante sana. What is the problem? Ulijiandikisha wakati gani?

**Speaker:** Nani mwingine anataka kwenda?

**Com. Paul Wambua:** No, those ones I have finished with them. According to me, huyu mzee alimaliza kuzungumza, huyu sijamwita maanake tulimaliza wale walikuweco...

**Interjection:** (Inaudible)

**Com. Paul Wambua:** Hapana. Tumemaliza Mzee, wacha tuwapatie wengine nafasi. Wewe umejiandikisha? Sasa how do we call you? You have not registered your name there. Who has registered his name and has not spoken now? Mzee, nitawapatia nafasi, sasa wa mwisho kabisa tutaenda hivi na msikize vizuri.

Utazugumza, huyu atafuata, na wa mwisho atakuwa ni District Coordinator Elija Letangula. That is the procedure na kila mtu apate three minutes, tumalize. Mfuatane hivyo hivyo.

**Pastor Aaron Kipsomet:** Basi, asante Mheshimiwa, mimi ni Pastor Aaron Kipsomet. Ninamaoni karibu manne.

Ya kwanza: Tumeona ya kwamba kuna shida ya watoto wetu ambao ni wasichana. Tukiangalia idadi ya wale wanaoingia shule kwa Primary, kwa kama class one, ni wengi lakini wakifika darasa la nane, ni wachache ambao wanaweza kufanya mtihani wa darasa la nane.

Shida ambayo inatokea ni ya kwamba kuna wasichana ambao katikati kwa shule ama hata kwa Secondary school wanapata mimba na wakipata mimba, hawa watoto wana akili lakini kwa sababu ya mimba...

**Com. Paul Wambua:** Unapendekeza nini?

**Pastor Kipsomet:** Ninapendekeza ya kwamba hawa watoto waruhusiwe waendeleo na masomo. Ikiwa ni shule hiyo ama ingine, waendeleo kwa sababu ya maisha yao.

Jambo la pili ni mambo ya kuwaajiri chiefs ama assistant chiefs. Tumeona ya kwamba watu siku hizi, assistant chiefs...

**Com. Zein:** Mzee wangu, pendekeza.

**Pastor Kipsomet:** Pendekezo ni hivi, ningependelea sana kama Assistant Chief ama Chief wangechaguliwa na watu.

**Com. Zein:** Watu wametoa maoni hayo na wengine wanasema wachaguliwe na mlolongo.

**Pastor Kipsomet:** Okay, haya. Lngine ni dini. Kenya kumekuwa na uhuru wa kuabudu lakini kuna dini zingine ambazo si halali. Pendekezo langu ni ya kwamba dini ambayo ni ya mashetani iondolewe kwa nchi yetu.

**Com. Zein:** Kuhusu uhuru wa kuabudu, iwekewe vikwazo kwamba watu wanaoabudu shetani wasiruhusiwe.

**Pastor Kipsomet:** Ndiyo. Jambo lingine la mwisho: Tumekuwa na pornographical books ama hii nauzwa kwa magazeti kila mahali na wanaenda kuangalia.

Pendekezo ni kwamba serkali ione ya kwamba pornographical video ambayo ni mbaya iondolewe kwa watu wetu.

Asante sana, ni hiyo niliyokuwa nayo.

**Com. Zein:** Asante sana. Tafadhali jiandikishe pale. Ndiyo, ndiyo. Kama unavyoona mwenzako tunavyomwambia, tunataka mapendekezo kwa sababu ukitupa hadithi, haingii kwa katiba. Mapendekezo yako ndiyo yanaingia kwenye katiba. Utaje jina uendelee.

**Weston Wanjohi:** Kwa majina ninaitwa Weston Wanjohi.

Langu la kwanza ningependekeza ya kwamba tuwe na a unitary form of government.

The Constitution inafaa kutu address as Kenyans and in that Constitution, the name of the Country should be changed in order to foster national unity.

**Com. Zein:** To what?

**Mr. Wanjohi:** To what? I suggest that the Country should be named the Democratic Republic of Kenya and that will also affect the Kenya currency.

Hii pesa yetu ya Kenya sasa inafaa ibadilishwe.

**Com. Zein:** Hapana Stories, pendekezo.

**Mr. Wanjohi:** Pendekezo yangu ni ya kwamba some changes should be made.

**Com. Zein:** Which changes?

**Mr. Wanjohi:** The face lift of the Currency.

**Com. Zein:** You are going to propose that we should not have images of persons on the currency?

**Mr. Wanjohi:** Yes. Not all the currencies, the major currency, the bigger currency inafaa kuwa na picha ya the current head of state,

**Com.?:** Sawa,

**Mr. Wanjohi:** Halafu the other currency inafaa kuwa na vitu ambayo iko na pengine uchumi, nchi na mambo yanahusiana na unity

**Com. ?:** Sawa.

**Mr. Wanjohi:** Halafu tukishuka chini kidogo kuna mambo kama ya appointment ya Auditor General, ya Attorney General, Commissioner of Lands, all those should be parliamentary appointees but not appointed by a person who is holding the office of

the President.

Another suggestion ni ya kwamba mambo kama office ya Attorney General. In the current constitution, role za AG ziko duplicated.

**Com. Zein:** Hapana, hapana. Pendekeza.

**Mr. Wanjohi:** Pendekezo yangu ni ya kwamba, the AG should not sit in the Executive government and at the same time acting as the government prosecutor.

**Com. Zein:** Are you proposing that we should ---(not clear) Attorney General?

**Mr. Wanjohi:** Yes that is my recommendation.

**Com. Zein:** The Prosecutor General should be the advisor of government and the minister for constitutional affairs.

**Mr. Wanjohi:** Yes.

**Com. Zein:** Sawa.

**Mr. Wanjohi:** Ya mwisho ni ya kwamba, because I believe that it is not the Constitution which wants us, it is us who want a constitution, so most of the things yanayofanyika inafaa iwe ni raia ndio wanaongoza. We want a government ambayo inahitaji raia, raia ndio wanaongoza so mambo mingi inafaa, kama mambo ya budget, raia wawe wanatoa views; economists wanatoa views vile budget ingetakikana kuwa.

Ninafikiri ni hiyo pekee yake.

**Com. Zein:** Asante sana. Kabla sijakuja kwa Coordinator...Mzee wangu, nikisema kabla sijakuja kwa Coordinator, ni ajie fursa nizungumze. Mimi sikuzungumza leo, mlinisikia nikizungumza?

**Audience:** (Inaudible)

**Com. Zein:** Basi nipeni fursa nizungumze kidogo. Kijana ulikuwa unataka kusema nini ambalo halijasemwa? Una mangapi? Kimbia basi mara moja, usimame pale. Mzee wangu, kaa karibu na yeye useme moja pekee yake kwa sababu umeshazungumza na sisi mara mbili, ukasema unaandika memorandum itakuja, kama umesahau jambo ni hili, sawa. Taja jina na useme.

**Raymond Cheboi:** Ninafikiri mimi kwa jina ninaitwa Raymond Cheboi. Nilikuwa nataka tukuanza kuangalia mambo ya documents, confidential documents. Kusema tu kuhusu documents zile za serikali. Unakuta zingine, tuseme kama zile za application... nilikuwa tu niseme kuna documents za serikali ambazo ni muhimu sana kwa mwananchi, kwa mfano ile ya application kwa upande wa kazi ya serikali na mengine. Ukikuta saa zingine hii documents inakuwa very scarce, yaani haipatikani kwa urahisi na ukipata moja unakuta inasema photocopies are not allowed na yule ofisa mkubwa anayepeana huko anasema ile shida iko...

Nilikuwa nataka tu niseme kuna sheria ingine ambayo...

**Com. Zein:** Unapendekeza karatasi muhimu za serikali ziwe --- (not clear) kwa mwananchi?

**Mr. Cheboi:** Ndiyo hiyo.

**Com. Zein:** Basi.

**Mr. Cheboi:** Asante. Halafu kwa upande mwingine ni autonomy ya Local Authorities. Nilikuwa ninataka kusema tu kuna serikali kuu na kuna serikali za wilaya. Ninataka kusema serikali kuu na hii serikali ya wilaya kwa hakika inatumikia mwananchi.

So tukija kwa service delivery, saa hii uzito sana iko kwa serikali kuu na tukija kwa serikali za wilaya unaona sana tunategemea...

**Com. Zein:** Unataka nini?

**Mr. Cheboi:** Tunataka Autonomy:

**Interjection:** (Inaudible)

**Mr. Cheboi:** Okay. Na nilikuwa tu ninataka kuongeza kwa mfano...

**Interjection:** (Inaudible)

**Mr. Cheboi:** Ni mawili. So ninafikiri, kulingana na vile mambo ya kuabudu, mimi ninamuunga mkono pastor aliyekuja kusema hapa ile sheria ya kuabudu iwe free lakini kama kuna mengine ambayo si mazuri kwa mwananchi hakika iwe restricted.

Kwa haya, asante.

**Job Seng'enge:** Asante sana Waheshimiwa Commissioners. Yangu ni machache ambayo.

**Com. Zein:** Taja jina.

**Job Seng’enge:** Jina ni Job Seng’enge, former Councillor. Asante sana.

Mimi niliona kwa upande wa President na Prime Minister vile Wakenya wataendelea kupendekeza, awe ni mtu kutoka miaka arobaini na tano na kuendelea. Isije ikawa ni kila mtu ataleta mtoto wake hata yule bado anamnyonya mama na kusema anakuwa President.

(Laughter)

**Com. Zein:** Mzee wangu, ngoja Mzee wangu. Siasa mimi sitaruhusu lakini... unajua mini ninakuheshimu sana Mzee wangu? Umependekeza kwamba Rais aanze kuchaguliwa akiwa na miaka arobaini na tano. Lingine,

**Mr. Seng’enge:** Asante Mheshimiwa.

**Com. Zein:** Lingine, Judge na waalimu wale wa Secondary ambao walisomea, pamoja na madaktari wakuu, wale wote ambao wana uchuzi waliosomea kwa muda mrefu, waendeleo mpaka miaka sabini kwa kazi yao. Sawa sawa, hata nyinyi vile vile, namna hiyo.

Na walimu wale wa Primaries waende mpaka miaka sitini.

Ya mwisho ni ya kwamba tulipopendekeza mambo ya majimbo, kuna neno moja ndani yake. Kuna katika Kenya, kati ya provinces yote nane, kuna provinces mbili ama moja ambayo tayari imefanya majimbo hawaruhusu jimbo lingine kufanya biashara katika area hiyo.

**Com. Paul Zein:** Tafadhalini, tunafaa tumsikize huyu anayetoa maoni.

**Mr. Seng’enge:** Ikiwa tu sitaji kwa sababu tukiwa katika Commission namna hii tunasema mnaelewa tu. Sasa ndiyo tunasema ili kufufua uchumi, ni rahisi watu wanapoketi chini, ikiwa ni province na kujifikiria vile watu wao watapona.

Asante sana, sina mengi. Nitatuma tu ile yangu. Asante kwa kuniheshimu hivyo.

**Com. Zein:** Asante Mzee.

**Com. Zein:** Mzee, hakuna mtu mwingine amepewa fursa mara mbili. Ngoja wale wamalize, ninamalizia na huyu halafu utaniambia kuna kitu kimekufanya ushindwe kulala.

**Elia Letangule:** Asante sana. Kwa majina ni Elia Letangule kutoka Marigat.

Pendekezo langu ni kwamba community ya Njemps, jina lake haswa ni Ilchamus. Pendekezo langu ni jina la Community ya Njemps, ambao wanaitwa Njemps ni kwamba hilo siyo jina hasa. I-L-C-H-A-M-U-S.

La pili: Njemps ni moja ya community ya Maa na tunavyojua, katika agreements za 1904 – 1911, Wamaa walipoteza nchi yao kubwa kwa wazungu. Pendekezo langu ni kwamba kama vile kuna kuwa na compensation, community ya Njemps wawe compensated kwa sababu ya hiyo nchi walipoteza wakiwa ndani ya community ya Maa.

Kwa ujumla, Maa community tunaomba tupewe compensation kwa ile ardhi, ile land, white islands ambayo ilinyakuliwa na Wazungu kutoka kwetu na hata baada ya uhuru hatukurudishiwa.

Pia, community ya Njemps ni ndogo sana katika Baringo district na hata wakipewa miaka mia moja hawatachagua MP. Ninapendekeza kwamba nominated MP iangalie watu kama hao because even if we are given a thousand years...

**Interjection:** (Inaudible)

**Mr. Letangile:** Small groups pia, kwa hivyo nominated Councillors waangalie vikundi ambavyo havitaweza, kama Waswahili hapa Kabarnet na Wanubi.

Asante sana.

**Com. Paul Wambua:** Basi, tumefika mwisho wa kikao hiki. Mzee bado ana insist. Mzee, hebu kuja, kuja hapa. Kuna shida gani? Sema.

**Speaker:** Asante sana kwa kunipatia nafasi ya pili. Kitu yenya ningetaka kuwaambia wananchi wangu hawa...

**Com. Paul Wambua:** Tunataka utupatie mapendekezo.

**Speaker:** unajua nyinyi ni wageni lakini mimi ni mwananchi wa area hii. Kitu yenye ilinibabaisha mpaka saa hizi, wewe ukiwa pale, hata na huyo, kitu yenye, mimi niliendanga shifta, Mzee yule hayati aliambiwa a-declare war huko Somalia. Akasema mimi watoto wangu ni wachanga, siwezi ku-declare war.

**Com. Paul Wambua:** Basi, basi.



**Speaker:** Basi, sasa nyinyi mtuchunge tafadhali.

**Com. Paul Wambua:** Tosha basi, tumesikia hayo.

**Speaker:** Mtuchunge tafadhali, don't even harass us.

**Com. Paul Wambua:** Haya! Asante sana.

**Speaker:** Asante sana. Hiyo ndiyo kitu ningetaka hata watu wajue; tumelindwa vizuri sana. Hata kama tuko maskini, tunaweza kuwa ndani ya kwapa tu ya mtu. Asante sana.

**Com. Paul Wambua:** Basi tumefika mwisho wa kikao hiki kuanzia asubuhi na sasa ningependa kirasmi kutaja ya kwamba sasa tutakoma hapo na kwa niaba ya Macommissioner wenzangu ambao hawajarudi hapa, walitoka, ambaye alikuwa mwenyekiti wa kikundi hiki cha Commissioners, Commissioner Pastor Zablon Ayonga na Mama Phoebe Asiyu. Na kwa niaba ya mwenzangu hapa, commissioner Zein, ningelipenda kuwashukuru nyote ambao mlifika hapa na kutoa maoni yenu.

Maoni ambayo mliyatoa ni ya maana na kazi yetu kama Tume ni kuhakikisha kwamba yale maoni yote ambayo yalitolewa hapa yataingia kwa reports; kwanza ya Constituency, ambayo tutaitengeneza na pili kwa ile report ya kitaifa ambayo tutatengeneza.

Kulingana na taratibu ambazo zimewekwa, tutamalizia hapa Rift Valley province ifikapo tarehe ishirini na saba mwezi huu, kumi na saba, si ishirini na saba, halafu tutaelekea huko Western Province na tunatarajia kwamba tutamalizia Western Province tarehe thelathini mwezi wa saba.

Tukimaliza Western Province, tutaanza shughuli kwanza ya kuandika report na report zitakuwa za aina mbili, kutakuwa na report ya constituency ambayo itarudishwa kwenu na mtaichunguza kuhakikisha ya kwamba yale yote ambayo mliyataja kweli yaliingia kwa hiyo report. Ikiwa kuna mambo ambayo mliyataja na hayakuingia kwa report, basi mtapewa na nafasi ya kutaja tena.

Halafu tutatengeneza pia ile report nyingine ya kitaifa, ikiwa sheria iliyoko sasa haitageuka, tutatakiwa tuirudishe kwenu tena muisome halafu mtupatie maoni yenu kwamba yale yote ambayo mliyataja kweli yako kwa hiyo report.

Pia tutatengeneza Katiba, Draft Constitution, na hiyo Katiba pia kulingana na sheria mtatakiwa muisome, mhakikishe ya kwamba inafaa kulingana na ile report ambayo tuliitengeneza na kulingana na maoni yenu.

Tutatakiwa tuipeleke kwa kikao maalum cha kitaifa, ambayo tunaita National Constitutional Conference, na kwa kikao hicho

kutakuwa na MPs ama all elected and nominated MPs, kutakuwa na Commissioners, wakiwa ishirini na tisa, kutakuwa na waakilishi wa vyama vya kisiasa, kutakuwa na waakilishi kutoka kila wilaya na hawa watachunguza na kwa kweli, katiba itatengenezwa kwa hiki kikao cha National Constitutional Conference.

Wakishakubaliana kwa ile Draft Constitution ambayo Tume itakuwa imetengeneza, basi hiyo itapelekwa huko Bunge na itapitishwa kuwa katiba mpya.

Ikiwa hawatakubaliana, sheria iliyoki inasema ya kwamba kuwe na referendum ama kura ya maoni ambayo wananchi sasa wataamua kwa yale mambo ambayo hawakukubaliana.

Basi ikipitishwa ama kura ikipigwa, Draft Constitution na maoni yenu yatapelekwa Bunge na Bunge itapitisha iwe Katiba Mpya.

Huo ndio basi utaratibu ambao tutafuata kuanzia leo na kwa hivyo tutarudi hapa hapa maanake sheria inasema turudi hapa kwenu tuzungumzie hizo report za Constituency na za kitaifa na wale ambao walikuwa wanafanya mambo kama 3Cs, nafikiria wako hapa, bado kuna kazi na hiyo kazi mtatakiwa muendeshe, mtatakiwa muwasomeshe wananchi kwa yale mambo ambayo yamebaki, stages zimebaki, reports ambazo tutaleta huku, halafu tutachukua maoni tena ya wananchi.

Kwa hivyo tungelipenda kuwatambua wale ambao walikuwa wanafanya kazi katika hii constituency ya Baringo Central. 3Cs wako wapi? Naambiwa wote wameondoka lakini hata wakiwa wameondoka, lakini tungependa kuwashukuru wale ambao walipanga mpango huu kuhakikisha ya kwamba kikao hiki kimefaulu na hawa ndio wale members of 3Cs, nafikiri pengine wametangulia huko Mogotio, maanake kesho tutakuwa huko Mogotio pia kuchukua maoni ya wananchi. Kwa hivyo kwa niaba ya Commissioners na kwa niaba ya Tume, tunataka kuwashukuru wote members wa 3Cs waliohusika kupanga kuhakikisha kwamba tumefaulu na pia District Coordinator ambaye alianza kufanya kazi, yeye ndiye field officer wa Commission, kuhakikisha ya kwamba pia tumefaulu katika wilaya ya Baringo, tungependa kumshukuru pia naye.

Sijui kama kuna member wa Provincial Administration hapa? Kama hayuko, asubuhi ya leo tulikuwa na DC. Ningelipenda kushukuru pia Provincial Administration maanake wao wametusaia sana kupanga huo mpango kuhakikisha kwamba vikao vyote katika wilaya ya Baringo vimefaulu.

Kwa hivyo kwa niaba ya Tume pia ningelipenda kuwashukuru Provincial Administration ama hiyo idara ya utawala.

Tumefikia mwisho sasa wa kikao hiki. Nitampatia mwenzangu Commissioner Zein kama angependa kusema machache halafu tutamuuliza mtu mmoja atuongoze kwa maombi halafu tutakifunga kikao na Mungu akitujalia, tutakutana tena kwa kikao kikingine. Hata ikiwa si cha Katiba, kingine tu.

Kwa hivyo Bwana Zein...

**Com. Zein:** Yangu yatakuwa machache sana. Ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru wakenya wote waliofika hapa,

hasa wakaazi na watu wa kutoka sehemu hii ya Baringo Central kwa kutoa maoni mazuri na maoni ambayo sisi tunawahakikishia tutayatumia kama nguzo na misingi ya kujenga Katiba mpya na kama alivyosema mwenzangu, hakikisho hilo mtalipata mtakapo angalia ripoti, muone kwamba ripoti ya constituency au ya sehemu ya uwakilishaji Bungeni ya sehemu hii imeonyesha mambo yale mliotueleza.

Na pia ningependa kutoa shukrani zetu nyingi sana kwa watu wa Baringo kwa sababu toka tulipofika hapa Baringo juzi, tukaanzia Baringo North na leo tumefika Baringo Central, mmetukaribisha kwa wema na tumekuwa na tumeishi hapa vizuri sana. Tumekuwa na raha nyingi sana na ukarimu wenu tutaukumbuka kwa muda mrefu sana na tutaondoka hapa na ukumbusho ambao hatutausahau hivi karibuni na pia sichoki kusema kwamba tumefurahi sana kwamba tumestaajabukuona jinsi mnavyolinda mazingira hapa na kwamba sehemu hii ni sehemu ya aina ya pekee katika jamhuri ya Kenya kwa sababu sisi tumetembea karibu nchi nzima sasa kama alivyosema, tumebakisha mkoa wa magharibi pekee yake, lakini hatujaona misitu yenye miti ya kiasili mingi kama tulivyoona huku.

Kila mahali tunapo angalia tunaona kijani tu, kijani kibichi.

Tunawashukuru sana na tunawapongeza na kuomba muendeleo na kazi hizo na tunaamini kwamba utamaduni wenu umewasaidia kuchangia kuwa na utunzi wa mimea na misitu ya aina hiyo kwa sababu hata mapendekezo tuliyopata, tumepata kwamba watu wanapendekeza mambo yanayofanyika hapa pia yafanyike sehemu zingine nchini na yalindwe kikatiba. Kwa hivyo tunashukuru sana.

Mwisho kabla sijakaa chini, ningependa kwa niaba yenu kumshukuru huyu dada hapa, huyu bibi aliyekuwa akitafsiri. Wengi wenu mnaona tu anatumia ishara. Ni muhimu sisi kueleza kwamba kama Tume ya kurekebisha Katiba, sisi ni taasisi ya kwanza katika taifa letu kusema kwamba ni lazima tuwe tunatumia lugha ya ishara, sign language, kama njia ya kuwafanya ndugu zetu ambao hawasikii waweze kufuatilizia mambo haya na waweze kuchangia mambo haya.

Kwa hivyo tunamshukuru sana kwa kazi aliyofanya. Kutoka asubuhi amekuwa akiendelea mpaka sasa na ndugu zetu toka asubuhi wamekaa wakisikiliza na walipopata fursa wakatoa maoni yao.

La mwisho kabisa, pia kwa niaba yenu, ningependa kuwashukuru wao. Njia ya kuwashukuru kwa sababu wengi mnazoea na mlikatazwa kupiga makofi, pengine kwao tuwapigie makofi.

(Clapping)

Tunashukuru sana. La mwisho kabisa, mimi ninafuata desturi zenu kwa sababu mtu anakuja anazungumza hapa anasema la mwisho, la mwisho kabisa, la mwisho kabisa, la mwisho kabisaaa, na mimi wacha niseme la mwisho kabisaa kwamba, kwa niaba yenu nawashukuru wafanya kazi wa Tume ya kurekebisha Katiba. Wamekuwa wakifanya kazi hii kwa muda mrefu lakini

hawajachoka na wanaendelea kufanya kazi hii.

Asanteni sana na Mungu awabariki.

**Com. Paul Wambua:** Basi tutakoma hapo. Nilikuwa nimekumbuka pia kuwashukuru hawa maanake niliangalia nikaona hakuna mmoja wao alitoka hapo na kweli wako na imani na shughuli hii ya kurekebisha Katiba maanake hakuna mmoja wao alitoka hapo. Nilikuwa nitaje lakini kwa sababu mwenzangu ametaja hayo, sitayarudia.

Kwa hivyo nitamuuliza mmoja wetu ambaye anaweza kutuomba, Pastor yuko wapi? Aje hapa atuombe halafu tutafunga hiki kikao cha leo.

**Pastor:** Tusimame kwa maombi. Basi tuombe.

*Baba Mtakatifu, Mungu Muumbaji, Mlinzi na Mwokozi wetu, tunakushukuru kwa jioni ya leo. Asante kwa kikao ambacho tumeketi tangu asubuhi tukizungumzia jambo kubwa ambalo linahusu nchi yetu na sisi kama Wakenya.*

*Tunashukuru kwa sababu kwa uwezo wako tumefikia mwisho. Asante kwa watumishi, Commissioners ambao wamejitoa katika kazi hii kubwa na tunawaomba upate kuwaongoza na wengine ambao wanashirikiana pamoja uwe nao hata wanapojiandaa kumaliza sehemu hii ya kwanza ya kutengeneza Katiba, upate kuwasaidia na kuwapatia afya, uwalinde katika kusafiri kwao.*

*Tubariki kama wenyeji wa Baringo ya Kati na uwabariki pia watu wote ambao tutashiriki katika kazi hii. Tulinde tunapoachana mpaka tutakapokutana tena katika mkutano kama huu maana tumeomba tukiamini kwa jina la Yesu ambaye ni Mwokozi wetu. Amina.*

#### *PRIVATE HEARING (ONE PERSON)*

**Com. Paul Wambua:** What is your name?

**Samwel Chepkole:** My name is Samwel Chepkole, Samwel Cheboi Chepkole.

**Com. Paul Wambua:** Why are you not willing to give your views in public?

**Mr. Chepkole:** It is because I feel it might not be very healthy for me thereafter. You not yet still in a very open system. Sometimes comes and complains that you have done something or you are into politics or something like that. But we really aren't into politics.

Since we are discussing a national issue, the awareness should have been raised amongst the people that everybody who has something to say should come, whether you are a teacher or something like that.

There is the thing of if you are a civil servant and so when we have normally left, you start talking with the politicians and so that is engraved in many people. I am sure you have witnessed that many civil servants are just on the sides.

**Com. Paul Wambua:** And why is it that you did not consider the alternative of writing a memo?

**Mr. Chepkole:** I was not even expecting to meet the Commissioners except for my Colleague here who we teach together. After talking, then I found out Commissioners were here then as I was expressing my points, he said why don't you call the Commissioners.

**Com. Paul Wambua:** So you were not aware there was a sitting today?

**Mr. Chepkole:** I heard of it last night only.

**Com. Paul Wambua:** I think what we could do is that we just ask you to give us those aspects which you consider to be sensitive and then you can take your time because there is still time upto 15<sup>th</sup> of this month.

**Mr. Chepkole:** I will be away, I will be in Nairobi.

**Com. Paul Wambua:** You write your memorandum and either you bring it to Nairobi or submit it to the District Coordinator because part of the reason you are giving us is that is you were not aware. If you were aware, you would have written and given us. This is something, which has been going on for quite some time, civic education and all that.

The visit here was also advertised extensively in the newspapers so the reasons I mean you are giving us sound to us partly you feel that you have been victimized partly because you are not aware.

Give us those aspects, which you thought maybe would not be spoken in public and then you can write because this questions and issues are many. May be you need to take time, go through each one of them and give your proposal accordingly. If we were to sit and listen to all that, it would take the whole day.

So give us those issues which you think could not be spoken out there and then take you time, write a detailed memo, there is still time upto 15<sup>th</sup> and submit it, either give it to the District Coordinator or a member of the 3Cs, the Chairman or bring it to Nairobi.

**Mr. Chepkole:** I think there are no issues that cannot be mentioned there except that my own responsibility and my work, so

I felt like if I speak very eloquently on issues, it can also implicate badly on me.

Let me give you the issue of Councillors or something like that...

**Com. Paul Wambua:** You should not worry about that because we have had DCs present views to us, we have heard DOs presenting views to us. A PC presented views to us, we have had a PS present views to us. The PS did not say he will just go out and get a written submission.

We are going to interview the President at some point. So you should not worry.

We have heard Headmasters. Yesterday we had formal presentation from KNUT in Baringo North. They sent the Secretary to come and present the views of KNUT and they made very, what you might consider political statements concerning salaries of teachers and so on and so forth, concerning enrollment of students from Primary to University level, funding and so on and so forth.

So I don't think should you worry about anything; you should not worry at all but since we are here, we can give you three minutes, four minutes and the other people can hear what you have to say.

**Mr. Chepkole:** Thank you very much for offering me the priviledge.

One issue I had is...

**Com. Paul Wambua:** Just repeat the name again... Samwel?

**Samwel Chepkole:** Samwel Cheboi Chepkole, Principal, Tenges boys.

**Com. Zein:** We normally record every session, so do not worry about it.

**Mr. Chepkole:** Okay. My main interest is on education; that if we can set centers of excellence per every division, where you have a very qualitative Secondary school that will give chances to areas that have not been priviledged to get education. Getting people qualifying for lucrative courses like Architecture, Engineering, Law and Medicine because as per the current set up, those communities that have had an early start normally do qualify and unless students have gone to other schools in those areas, there own schools can not give them a chance.

For example, when you look at North Eastern Province, in 1999-2000, not even one single candidate had sat for Physics and therefore that means they are technologically disadvantaged.

An area cannot change, transform its own socio-economic situation if some of their own people have not reached a very high

level as far as education is concerned.

I also suggest that if we could have funding of education upto form four that would better be the basic education for Kenyans. After that they can go through their loans.

**Com. Zein:** Are you proposing free education upto form four?

**Mr. Chepkole:** Education for all to form four free for every one. That is what I am trying to suggest.

The other issue is on the institution of Chief: Where the chief should be of higher education, say a minimum of form four, perhaps a C or C+ and should have undertaken a training, preferably teaching or pastorhood so that we have people who can understand the perception of the moment in terms of world trends unlike now where we have many illiterate chiefs who will rule may be more through the muscle and then there is no understanding. So if the chiefs can be developed in terms of...

First of all you are a professional, you have a minimum of four and then from there you have a syllabus, training programme for chief on running of public affairs in there locality, that would be okay, it will assist because in most of our cultures, the traditional set-up is gone but we must have somewhere to lean on.

When you leave it to the politics where you say let the leader be the one elected, then there will be a lot of politicking around and the issues are not addressed. It will be just mudslinging, talking about one another and so we do not have somebody to look to like the church and the stable administration.

Those are some of the things I thought I would say.

The land issue: Land should not be limited in terms of how much one owns. What we would have done according to me is maybe develop infrastructure to as many places of the country as possible and let people come out of the urban area.

If it is a local center, let them be more there then provide facilities in that set up where you have a school, you have water, you have health, and you have all those. That will make many people come to the market, they get to technology, they get to the power line, they get quality education, they start businesses and they will not refer to the land.

That way you will have those who can specialize in farming or any other activity doing it, of course alongside the state. There is the individual who is very good in that area and then the state; of course the overall overseer of land.

The other issue is on the environment: As far as the environment is concerned, because I look at Kenya now, we are very polluted. We have put rubbish even in front of our shops and we have destroyed the forests so the lungs which would give us

fresh air... so I was suggesting if we can have environment and natural resources as a subject, we develop a syllabus for that area to be taught at Primary, Secondary upto university level.

First it should be compulsory at Primary and Secondary because it is a relevant subject.

If we are telling a country let us have industrialization by the year 2020, industries definitely will bring pollution and that pollution will affect the state of our health and if that is so, then the environment component should go alongside the industrialization efforts we are trying to make.

You can be a professor of environment but you are living in a very dirty atmosphere because rain falls, it carries all the dirt and causes Typhoid, Amoebiasis among the people therefore the government will spend a lot of money on health to treat this people but if they all were environmental conscious, they would have known how to keep their wastes, to dump them in the right place, clean them and the way they stay, trees and all these.

For these to happen better, when that has been done, I wish that the natural resources and environmental issues, particularly the forests, may be mineral resources or wildlife, the local community should have a share of ownership so that they do not destroy because when they know it contributes to their lives, then they will definitely protect and by protecting they know they will have money to educate their kids, they will have money maybe for the common facilities, they will have some of their own employed there, along the state management.

I wish that the ownership is both community based and state.

Community may be at the local level could be the Local government or any other set-up that we think is functional for the management of our natural resources. Otherwise, as it is now, you will find that it is state owned. Somebody is sent from Nairobi to this place then he just finishes the forests and goes away and the elders have been here for ages and they have not destroyed so when they see somebody coming in within one and finishes the forests, they see that we better even benefit ourselves; we have taken care of it and somebody has just taken it.

That has led to fast rate of the depletion of our forests.

On water management: You look at it that we don't have enough safe waters. Maybe one percent of the world's water is clean drinking water. A way should be found out because as you can see, through this environmental problem, we are manufacturing water and we are selling it now at the shops. What will happen to those people who will not afford? Can we set up structure in place that can save the ordinary people so that they have at least access to clean drinking water because most of the diseases that people suffer from are water-borne?

The component of the environment and water is what can help better health than most of the money that would have been used to treat, can be used to create job opportunities or economic activities that can help our country to prosper in a very healthy atmosphere because you can be progressive industrially but people are not healthy, that would not be good.



And then the issue of governance as far as the state is concerned: I would have wished that... In 1997 you remember very well that we were saying no reforms, no budget, at one stage we almost went without a budget. I think you remember if you were following what the parliamentarians were doing to the extend of fighting.

Then the next one came; no reforms, no elections. I would wish that in the coming election, can we do it on a new constitution so that the dissenting voices, those who were dissenting in 1997, if they were genuine and good leaders, they will definitely be elected.

Otherwise, they would look like they had no reason, it will look like they were either focusing on the President, the current President or they were just interested in selfish things.

At least if we have the new Constitution, because everybody has participated, I can see ufungamano was there, the opposition was there, KANU was there and now professionals have been brought in to steer this thing through. Therefore, if it can be done on a new Constitution, then it will be okay. Otherwise, it will look like the current Constitution had no problem if we have to do it on this Constitution yet we were complaining before that.

Those are really some of the things that I thought if we can look at, we would be okay.

On election of Chairmen of County Councils, I would prefer that they be electable by the electorate themselves and not there Councillors because they are bought and they compromise their position and therefore they may not represent the interests of the people.

Another issue is if we can have two Houses of Parliament, may be a Lower House or a Upper House, whichever the name is because there are small communities that currently cannot be represented by the current set up because of majoritarian dictatorship because...

**Com. Zein:** That we understand. If you give us a principle we write if down. You want a bicameral system, fine.

**Mr. Chepkole:** Fine. I don't know what you ... I was just...

**Com. Zein:** A two-chamber House.

**Mr. Chepkole:** A two-chamber House...

**Com. Zein:** The reasons are very clear to us.

**Mr. Chepkole:** Okay. I don't have anything more as far as my issues are... those are the basic things I would have asked in the Commission.

**Com. Paul Wambua:** I still think what you could do Bwana Chepkole is, find time, see what other issues you can still write. I am still saying that there is time to contribute, because your suggestions are very very sensible, so why don't you find time, go through this, and give us a proposal on some of the issues that you have not covered.

You still can submit that memorandum to us before 15<sup>th</sup> and then it will be taken into account but these ones have already been picked, haphazardly

**Mr. Chepkole:** Okay. I had something on infrastructure, could it also...

**Com. Wambua:** I was saying you can write really. These are the things, which you thought you could tell us now and we have given you even more than the time that we were giving the other people.

**Mr. Chepkole:** I am very grateful.

**Com. Paul Wambua:** If there are other issues that you still feel have been left, please address and write. I do not know why you are fearing to write. Just write and give it to the Coordinator. Anything given to us is given in confidence, we do not disclose names of people. All we are saying is that let us have whatever proposals you have on each of these issues if it is not covered here.

**Mr. Chepkole:** Okay.

**Com. Paul Wambua:** Okay, thank you very much.

**Mr. Chepkole:** Thank very much Commissioners. Thanks for your kind consideration, otherwise I would have just...  
Asante.

